

# Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA TOLEO LA 2 & 3, 2013 Bei Sh. 500

MIAKA  
**50**



## TOLEO MAALUMU

Jipatie nakala yako ujue mambo mbalimbali kama vile:

- Faida za kuwa na Kanisa nchini
  - Utambulisho wa KKKT
  - Maana halisi ya 'Ulutheri'

Vol. 113, Namba 2 & 3, 2013

ISSN 0856 - 1214

**JUBILEE YA KKKT**

# Lutheran Uhuru Hotel and Conference Centre



Mandhari ya Kuvutia



Malazi Safi



Nyamachoma Maarufu



Vyakula vya Kikwetu na Kigeni

Kwa Mikutano, Semina, Harusi, Malazi, Mapumziko na Nyamachoma  
Pia Tunapeleka Wageni Mlima Kilimanjaro na Mbuga za Wanyama

*Ukihitaji Maelezo Zaidi, Wasiliana na Meneja*

Lutheran Uhuru Hotel & Conference Centre

P.O. Box 1320, Moshi, Tanzania: Simu: +255 272 754 084; +255 753 037 216  
e-mail: [reservation@uhuruhotel.org](mailto:reservation@uhuruhotel.org); [manager@uhuruhotel.org](mailto:manager@uhuruhotel.org)  
[www.uhuruhotel.org](http://www.uhuruhotel.org)

## Huduma za Uchapishaji

Moshi Lutheran Printing Press ni kiwanda chako cha uchapishaji kinachoongoza kote kaskazini ya Tanzania kuhusu ubora, unafuu wa gharama, kasi na uaminifu. Tunachapisha:-

Vitabu, Kadi za kila aina, Majarida na Magazeti, Mabango, Vipeperushi,  
Bahasha, Hati za Fedha, Tikiti, Ratiba, Pakiti, Majalada, Daftari, n.k.

Tunatoa huduma kamili za typesetting na usanifu.

Tunakarabati vitabu vichakavu vikawa vipyta tena.

Kwetu hakuna kazi iliyo ndogo mno au kubwa mno.

Tunakushauri kuhusu kufanikisha malengo yako.

### *Fika Mara Moja*

MOSHI LUTHERAN PRINTING PRESS  
S.L.P 301, MOSHI, Simu: +255 272 750 546  
E-mail: [lutheranpress@yahoo.com](mailto:lutheranpress@yahoo.com)



Uhuru na Amani ni Gazeti la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hutayarishwa na Kitengo cha Mawasiliano, KKKT.

Maoni yaliyomo katika makala zinazochapishwa ni ya mwandishi anayehusika na wala hayawakilishi mawazo ya Kanisa ama mhariri isipokuwa pale ambapo imetamkwa wazi.

Ukiwa na maoni, ushauri, makala au maswali mwandikie:

**Mhariri**  
**Uhuru na Amani**  
**S.L.P. 3033, ARUSHA.**

**Barua pepe:** elobulu@elct.or.tz  
sms kwa Mhariri: 0754-482-285

**Fungua Tovuti ya KKKT:**  
<http://www.elct.org/>

**Limepigwa chapa na**  
ELCT ND Moshi Lutheran Printing Press  
**S.L.P. 301, MOSHI.**

**MHARIRI**  
**Elizabeth Lobulu**

### **Waliochangia makala:**

**Askofu Elisa Buberwa**

**Mchg. Pro. Joseph Parsalaw**

**Mchg. M. Scheckenbach**

**Mchg. Dkt. Elieshi Mungure**

**Frederick Nzwili**

**Patricia Mwaikenda**

**Dkt. Geofrey Sigalla**

**Askofu Dkt.O. Mdegella**

### **PICHA YA JALADA:**

**Kulia ni Askofu Dkt. Alex Malasusa, Mkuu wa KKKT tangu 2007. Kushoto ni Hayati Askofu Dkt. Stefano Moshi, Mkuu wa KKKT 1963 - 1976.**

# **MAONI YA MHARIRI**

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) tarehe 23 Juni 2013 liliadhimisha kilele cha jubili ya mwaka wa 50 tangu makanisa saba ya Kilutheri yaliyokuwepo yalipouna na kuunda kanisa moja la Kilutheri nchini. Makanisa hayo kwa umoja yaliunda Katiba moja na vyombo vya uongozi na maamuzi. Taswira ya KKKT ina lengo la kujenga: “*Usharika wa watu wenyewe upendo, amani na furaha, waliobarikiwa kiroho na kimwili, wenyewe matumaini ya kuurithi uzima wa milele kwa njia ya Yesu Kristo.*”

Hivyo si rahisi kuwa ni nafasi ya kutosha katika gazeti hili kuelezea kazi zote au huduma zote za kiroho na za kijamii zilizofanyika kutekeleza *Utume wa Mungu kwa Kanisa wa kueneza Injili* kwa kumhudumia mtu kiroho, kiajili na kimwili kwa kipindi cha miaka 50 ya kuungana kwa KKKT. Mengi yamefanyika kutekeleza wito wa Kanisa kama inavyojidhahirisha katika dhamira yaani: “*Kuwa fanya watu wote wamjue Yesu Kristo ili wawe na uzima tele, kwa kuwahubiria Habari Njema kwa maneno na matendo, kwa kuzingatia Neno la Mugu kama lilivyo katika Biblia na misingi ya mafundisho ya Kilutheri kwa kuongozwa na Katiba ya KKKT.*”

Makala katika toleo hili yanaeleza kuhusu mipango katika kutoa huduma za kiroho, kijamii, kiuchumi na kuhifadhi mazingira; Kazi za misioni ndani na nje ya mipaka ya Tanzania kwa mbinu na njia mbalimbali kwa kupitia Dayosisi na Vituo vyake vya *Kazi za Umoja*.

Kanisa limefanikiwa katika kazi zake kwa sababu ya ushirikiano uliokuwepo kutoka kwa viongozi, Washarika na Vyama na Makanisa yaliyoingiza Injili nchini ambavyo kwa namna ya pekee vilipoona KKKT imeungana na vyenyewe vilikubali kuweka tofauti zao kando na kuungana ili kufanya kazi pamoja mionganoni mwa Watanganyika baadaye Tanzania.

Kutokana na hitaji la watendakazi, waasisi wa Kanisa hasa wamisionari *waliopanda mbegu ya Injili* walianzisha vituo au stesheni za misioni ambapo lilijengwa kanisa, shule na zahanati. Hatimaye vituo vikubwa zaidi vimejengwa na hadi mwaka 2013 Kanisa lina vituo vya mafunzo kama vile shule za msingi, shule maalum, sekondari, vyuo vya kati na hadi sasa kuna vyuo vikuu vya Kanisa vyenyeye kufundisha theology, fani za sayansi na sayansi jamii, nk.

Ofisi kuu za Dayosisi na Kanisa pamoja na mambo mengine zina jukumu la kuratibu kazi pamoja na kujenga uwezo kwa watumishi kwa njia za semina, mikutano na mafunzo mbalimbali; kufanya utetezi na kurahisisha utekelezaji wa mipango. Katika kurasa za toleo hili kuna taarifa jinsi Chuo Kikuu cha Tumaini kilivyoanzishwa; baadhi ya miradi ya kanisa ya kuondoa umaskini kama vile ufugaji ng'ombe wa maziwa, nguruwe na sungura na kuwezesha watu waanzishe ujasiriamali mdogo mdogo kuinua kipato; Huduma za tiba zilivyopanuka na kwamba Kanisa lina hospitali 23, hivyo kutoa mchango mkubwa sana katika sekta ya tiba nchini.

Kwa kiasi kikubwa sana katika maeneo ya utekelezaji wa miradi na mipango hii ya kijamii na kiuchumi inayosimamiwa na Kanisa huduma zinatolewa kwa watu wote bila ubaguzi wa dini zao. Tunawatachia wana KKKT heri kwa kutimiza miaka 50 ili Kanisa liendelee kuwa na umoja kama ulivyo wito wa Bwana Yesu: “*Wote wawe na umoja*”, Yoh 17: 21.

# Wageni 5000 kuhudhuria kilele cha jubilii



## *Na Elizabeth Lobulu*

Wageni wapatao 5,000 wanatarajiwa kuhudhuria matukio ya kilele cha jubilii ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) tarehe 22 na 23 Juni 2013 kukumbuka miaka 50 tangu makanisa saba ya Kilutheri nchini kuungana na kuunda kanisa moja.

Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa alisema hivi karibuni, kilele kitaadhimishwa katika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (Tumaini University Makumira -TUMA), Usa River kinachomilikiwa na KKKT kitakuwa na matukio ya siku mbili.

Alisema Juni 22 litakuwepo kongamano ambapo mada tano zitajadiliwa kuhusu kazi za Kanisa miaka 50 iliyopita na nini kifanyike kwa miaka 50 ijayo. Siku ya Jumapili 23 Juni ndipo itafanyika Ibada.

Kanisa linatarajia wageni wapatao 5,000 toka ndani na nje ya nchi kuhudhuria maadhisho hayo yatakayofanyika Usa River, nje kidogo ya jiji la Arusha. Wageni wa nje ni kutoka makanisa na vyama vya misioni vya Afrika, Ulaya na Marekani. Kutoka ndani ni pamoja na wawakilishi wa Dayosisi za KKKT, viongozi wa Serikali na wa dini na kwaya.

Chuo cha Makumira ni mojawapo ya vituo vya pamoja kama Kanisa (vijulikanavyo kama vituo vya Kazi za Umoja KKKT) kinachounganisha dayosisi zote 22 za KKKT. Ni kituo cha mafunzo kilichoanza kama chuo cha Theologia hivyo viongozi wa kanisa wakiwemo Wachungaji na Maaskofu wamesoma katika chuo hicho.

KKKT ni muungano wa makanisa saba ambayo baadhi yao yalianza

kutekeleza utume wa Mungu wa kueneza Injili nchini zaidi ya miaka 150. Tarehe 19 Juni 1963 viongozi wa makanisa hayo saba kwa hiari yao waliweka tofauti zao kando na kuamua kuunda Kanisa moja na kugeuza makanisa yao kuwa sinodi au dayosisi za KKKT.

Kadiri muda ulivyokwenda KKKT ikakubaliana kuacha mfumo wa sinodi na kuwa na mfumo wa Dayosisi. Hadi 26 Mei 2013 Dayosisi za KKKT zimefikia 22 baada ya mbili kuzinduliwa mwaka huu wa Jubilii. Nazo ni Dayosisi ya Kusini Mashariki (Mtwara/ Lindi) iliyozinduliwa Jumapili 26 Mei 2013 na Dayosisi Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria (Shinyanga/ Simiyu) iliyozinduliwa 5 Mei 2013.

Picha hapo juu inamwonesha Katibu Mkuu wa KKKT Bw. Brighton Killewa (wa tano kulia) akiwa na Makatibu Wakuu wa Dayosisi za KKKT.

## Makumira mwenyeji Jubilii ya KKKT



**Mchungaji Profesa Joseph Parsalaw  
Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha  
Tumaini Makumira (TUMA).**

Maandalizi yote yamekamika ya kupokea mkusanyiko mkubwa wa wageni toka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kilele cha kumbukumbu ya miaka 50 ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri nchini.

KKKT ni Muungano wa Makanisa saba ambayo baadhi yameshafanya kazi ya *Utume kwa kupanda mbegu ya Injili* nchini kwa takribani miaka 150.

Neno Kuu la Mkutano ni: *Wote wawe na umoja*, Yohana 17: 21.

Akielezea furaha kwa kuteuliwa kuwa wenyeji wa jubilii ya KKKT; Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA), Mchungaji Profesa Joseph Parsalaw, alisema chuo kinaona

fahari kutekeleza maono ya Kanisa kuteua Makumira kuwa mwenyeji wa matukio muhimu ya kihistoria KKKT.

Hata hivyo aliongeza kwa kuwa chuo kiko karibu na Ofisi Kuu ya Kanisa nayo ni mwenyeji na maandalizi yamefanyika kwa ushirikiano wa karibu na Ofisi Kuu ya Kanisa.

Profesa Parsalaw alisema KKKT iliundwa mwaka 1963 na mionganini mwa matunda ya umoja huo ni vituo vya umoja na Makumira ni kituo kimoja wapo cha umoja.

*Maelezo zaidi kuhusu Makumira yako kurasa za katikati katika toleo hili.*



# Dayosisi 2 zimezaliwa mwaka wa Jubilii

Nilipo mwomba hivi karibuni Askofu Mteule Lucas Luhigilo Judah Mbedule wa Dayosisi ya Kusini Mashariki anipe maoni yake kuhusu jubili ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), alisema bila kusita na kwa furaha kwamba ye ye ni tunda la miaka 50 ya KKKT.

Askofu Mbedule aliwekwa wakfu katika Usharika wa Mtwara tarehe 26 Mei 2013 kuwa Askofu wa Dayosisi ya 22 ya KKKT.

Askofu Mbedule alizaliwa 7 Julai 1965 Kijiji cha Lwang'a Wilayani Mufindi Mkao wa Iringa na kusoma Shule ya Msingi Udumuka alikohitimu mwaka 1982 na ana Stashahada ya Theologia toka Chuo cha Kidugala 1988 hadi 1999. Kwa sasa ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu Huria.

Alibatizwa 18 Agosti 1965 Usharika wa Kasanga na alibarikiwa kuwa mchungaji 30 Mei 1993 Usharika wa Kidugala. Askofu Mbedule amemwoa Mary Magava na kwa pamoja wana watoto watatu wakiume mmoja na wa kike wawili.



**Waziri Mkuu Mhe. Mizengo Peter Pinda akiwa katikati ya Askofu Lucas Mbedule (aliye na fimbo) na Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, katika picha ya pamoja na Maaskofu walioshiriki ibada ya kuwekwa wakfu Askofu Mbedule kuwa Mkuu wa Dayosisi ya Kusini Mashariki. (PICHA: © 2013 /KKKT)**

## Mchg. Makala awa Askofu



**Askofu Emmanuel Makala  
Dayosisi Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria.**

©KKKT 2013 (PICHA NA PHILEMON FIHAVANGO)

Tarehe 5 Mei 2013 Dayosisi Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria ilizaliwa. Mchg. Emmanuel Makala alibarikiwa kuwa Askofu wa kwanza wa Dayosisi hiyo mpya ya KKKT katika Usharika wa Ebenezar mijini Shinyanga.

Askofu Makala alizaliwa 6 Agosti 1964 Kijiji cha Kiziga, Wilayani Iramba Mkao wa Singida na kusoma Shule ya Msingi Yalagano mkoani Singida 1976 – 1983 ndipo akaingia Seminari Ndogo ya Kilutheri Morogoro (LJS) 1986 – 1990 hadi Kidato cha Nne na Kidato cha Sita alisoma hapo hapo 1991 – 1993.

Alijiunga Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira kwa mafunzo ya Shahada ya Mambo ya Dini (Divinity) 1994 – 1999 na alibarikiwa kuwa Mchungaji Septemba 1999 Usharika wa Mwadui alipokuwa mtumishi wa Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria ambapo alihudumu sharika mbalimbali 1999 – 2004 kabla ya kwenda tena Makumira kwa ajili ya Shahada ya Uzamivu katika Theolojia 2004 – 2007.

Baada ya kutunukiwa shahada yake ya Uzamivu alihudumu katika Usharika wa Kilutheri Shinyanga 2007 – 2008 na alikuwa pia Mkuu wa Jimbo la Kusini katika Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria.

Kuanzia 2008 hadi Desemba 2012 alikuwa **Dean** wa Kanisa Kuu la Kilutheri Mwanza na Desemba ndipo alichaguliwa na Mkutano Mkuu wa Dayosisi hiyo Teule ya Kusini Mashariki mwa Ziwa Victoria kuwa Askofu mteule. Tangu 2011 alijiunga na Chuo cha Concordia Seminary, cha Marekani kwa masomo ya juu yaani “Doctor of Ministry studies”.



**MIAKA  
50**

**Tunajivunia  
umoja si  
kwetu pekee  
yetu, bali  
umoja pia ni  
kwa vyama  
vya misioni  
ambavyo  
vina-  
fanyakazi  
Tanzania -  
Mkuu**

# Nguvu ya Kanisa ni katika umoja

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) linaposherehekea jubilii ya miaka 50 si ya kuingia Ulutheri bali ni miaka 50 ya makanisa saba ya Kilutheri yalipoungana na kuanzisha kanisa moja nchini. Injili ilienezwu kwa mara ya kwanza na wamisionari wa Kilutheri tangu 1887 katika eneo la Kigamboni, Dar es Salaam katika Dayosisi ya Mashariki na Pwani.

Makanisa saba ambayo hatimaye yaliunda kanisa moja mwaka 1963 ni Kanisa la Ubena-Konde (Nyanda za Juu Kusini); Kanisa la Uzaramo-Uluguru; Kanisa la Usambara-Digo; Kanisa la Kaskazini; Kanisa la Mbulu; Kanisa la Iramba-Turu na Kanisa la Kaskazini Magharibi.

Katika mahojiano na mwandishi wa makala haya hivi karibuni Mkuu wa KKKT, Askofu Alex Malasusa, alisema: "Tumefanikiwa mengi katika muungano kuliko tungebaki tumetengana."


Moja ya mafanikio makubwa ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ni kufaulu kuwa na Katiba moja iliyotokana na makanisa saba yaliyoungana miaka 50 iliyopita hadi sasa tuna Dayosisi 22.

Tunajivunia umoja si kwetu pekee yetu, bali umoja pia ni kwa vyama vya misioni ambavyo vinafanyakazi Tanzania. Tofauti na kabla ya KKKT kuundwa vyama vya misioni vilipoingia eneo fulani kila chama kiliendeze na kilishikilia

mtizamo wa Kanisa dada.

Tulipoungana tukafanya na vyama hivyo vielewe umuhimu wa kuungana. Kupitia chombo kilicho julikana kama LCS na baadaye LMC tunajadili, kupanga na kutekeleza miradi ya kijamii kwa sauti moja kama Kanisa katika vikao vya pamoja na makanisa na vyama vya misioni.

Uamuzi wa kuungana kama Kanisa baadaye makanisa dada ambayo hapo mwanzo hayakuwa na umoja nayo yalianza kufanya kazi pamoja na KKKT - Tanzania na kwinge duniani. Ni katika umoja ndio mambo makubwa yameweza kufanywa na KKKT, alisema Askofu Malasusa ambaye ni Makamu wa Rais (Kanda ya Afrika) wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani.



Mkuu wa KKKT ambaye pia ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Askofu Dkt. Alex Malasusa, akimwagilia maji mti alioupanda kama sehemu ya matukio ya kuzindua Kituo cha TUMA Mbeya (jengo hapo juu) 03 Machi 2013. Anayemshuhudia ni Mkuu wa Dayosisi ya Konde, Askofu Dkt. Israel-Peter Mwakyolile ambaye anaonekana picha ya chini akisoma Biblia. Kulia ni Mchg. Dkt. Gwamaka Mwankenja Makamu Mkuu wa Chuo hicho ambacho kinaandaliwa kupandishwa hadhi na kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Nyanda za Juu Kusini (*Southern Highlands University College*).



# WASHIRIKA

MIAKA  
**50**



Katika umoja ndio sababu KKKT imepiga hatua kubwa na mafanikio mengi yameonekana. Picha hii ni ya washiriki wa mikutano ya LMC ambapo washirika wa KKKT huja pamoja kila mwaka kwa majadiliano na viongozi wa Kanisa kupanga kwa pamoja masuala ya masomo, miradi, wamisionari, mbinu za utekelezaji na ufuatiliaji. (c) 2012 KKKT/ Picha na Michael Shao.

## Njiani pamoja kwa miaka 50



*Mwandishi wa makala haya ni Mchg. Manfred Scheckenbach (pichani juu), Katibu wa Afrika wa Kanisa la Kinjili la Kilutheri la Bavaria, Ujerumani.*

Mwaka 1962, kabla Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) halijaanzishwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la Bavaria, Ujerumani lilikuwa na uhusiano na Sinodi ya Kanisa la Kilutheri Kusini mwa Tanganyika.

Jubilii ya miaka 50 ya KKKT ambayo inasherehekewa na Dayosisi zote za KKKT, ilisherehekewa mwaka 2012 wakati viongozi walipotia saini hati ya makubaliano ya kuanza uhusiano baina ya makanisa haya mawili yaani Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Malasusa na Mkuu wa Kanisa la Bavaria Askofu Mkuu Landesbischof Dkt. Bedford-

Strohm.

Makubaliano hayo ni katika dhana ya ushirikiano miongoni mwa wanachama wa Lutheran Mission Cooperation (LMC) ambapo Kanisa la Bavaria linashiriki kikamilifu kwa kutoa karibu nusu ya fedha zinazohitajika za programu muhimu inayofahamika kama "ELCT Core Programmes".

Kwa sasa Kituo cha Uhushiano, Maendeleo na Misioni (MEW) cha Kanisa la Bavaria kimetuma Wamisionari kujaza nafasi saba katika nyanja za kazi za Kanisa na Maendeleo pia imewatuma watu 10 wanaojitolea. Mchg. Emmanuel Kileo na Mwanasheria Aneth Lwakatare wanafanya kazi Kanisa la Bavaria. Kwa muda wote pamekuwapo na mabadiishano ya watumishi

na wanatheologia wengi wa KKKT ambao wamepata mafunzo yao ya Uzamivu (PhD) Bavaria wanatumika katika nafasi za ngazi za juu KKKT. Zaidi ya makundi 30 baina ya makanisa haya mawili yanaendeleza uhushiano. Maeneo ya uhushiano ni pamoja na kueneza Injili, udiakoni, huduma za jamii na maendeleo na utetezi.

Haya makanisa yetu yanafaidika katika ushirikiano tulionao katika utume wake Mungu na nimefurahi kwamba nimehusiska katika uhushiano huu. Nilikuwa Mmisionari Tanzania kwa miaka minane. Natumikia kama Katibu wa Tanzania katika Kanisa la Bavaria nafasi niliyonayo kwa miaka 13 sasa.

*Mungu aendelee kubariki mapito yetu ya pamoja katika kutekeleza utume wake.*



# WASHIRIKA

## Marangu mwenyeji wa uzinduzi wa karne ya matengenezo Afrika

Na Fredrick Nzwili, Nairobi

Kilele cha Jubilii ya miaka 60 tangu viongozi wa Makanisa ya Kilutheri Afrika wakutane Marangu, Kilimanjaro; kitafanyika mwaka 2015 kuzindua matukio ya kukumbuka miaka 500 ya **Matengenezo** barani Afrika.

Makanisa ya Afrika ambayo ni wanachama wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) yamepatana katika kikao chao kilichofanyika mwishoni mwa mwezi Mei jijini Nairobi, Kenya kwamba Marangu iwe mwenyeji wa mkutano huo wa viongozi wa Afrika ili kukumbuka mkutano wa kihistoria wa 1955 wa makanisa yote ya Kilutheri Afrika.

Katika hotuba aliyoitoa katika kikao cha Nairobi, Makamu Mkuu wa FMKD Kanda ya Afrika, Askofu Dkt. Alex Malasusa, alisema upo uhusiano wa karibu kati ya kumbukumbu ya mwaka wa 60 wa mkutano wa Marangu na kumbukumbu ya matengenezo. "Ni muhimu kuhuisha, kuongeza nguvu na kuendeleza Makanisa barani Afrika kama ilivyojadiliwa miaka mingi iliyoleta pale Marangu," Askofu Malasusa alisema.



**Idadi ya wajumbe wanawake katika vikao vya maamuzi inaongezeka siku hadi siku kama inavyoonekana pichani juu wakati wa Mkutano wa Halmashauri Kuu ya KKKT 2013. Idadi ya Wachungaji wanawake imefikia 200 mwaka 2013 kati ya Wachungaji wapatao 2,000 KKKT.**

Mchg. Musa Filibus kuwa askofu

Mchg. Dkt. Musa Panti Filibus, (pichani chini) aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Misioni na Maendeleo ya Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), ameteuliwa na Kanisa la Kilulutheri la Kristo la nchini Nigeria (LCCN) kuongoza Dayosisi ya Mayo Belwa katika jimbo la Adamawa, Kaskazini Mashariki ya Nigeria.



**Mchg. Dkt. Musa Panti Filibus**

Filibus alijunga na FMKD Septemba 2002 kama Katibu wa Afrika na aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Misioni na Maendeleo Desemba 2010.

Na kutokana na mabadiliko ya mfumo wa uongozi wa FMKD aliteuliwa mwaka 2010 na Halmashauri Kuu ya FMKD kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Fungamano hilo lenye makao yake jijini Geneva, Uswisi.

Kanisa la LCCN lina washarika milioni mbili na ni moja wapo ya makanisa mawili yaliyo wanachama wa FMKD nchini Nigeria. Kanisa hilo lina dayosisi nane, eneo moja la misioni na linaongozwa na Askofu Mkuu Nemuel A. Babba.

Dkt. Filibus atawekwa wakfu kuwa Askofu wa kwanza wa Dayosisi ya Mayo Belwa mwezi Oktoba 2013 wakati wa jubilii ya miaka 100 ya LCCN. Dayosisi hiyo iliundwa mwaka 2011 na inazo sharika 300 na Wachungaji 60.

Filibus (53) alibarikiwa kuwa mchungaji wa LCCN mwaka 1994. Alisomea theolojia nchini Nigeria na Marekani na alihitimu hadi Shahada ya uzamivu ya udakatari katika theologia (PhD in pastoral theology). Amemwoa Mchg. Ruth Filibus na wamejaliwa watoto watatu. (LWI, GENEVA)

# VIONGOZI WA KKKT 23 JUNI 2013



**UMOJA**

**MIAKA  
50**

**Askofu Dkt. Alex Malasusa**


Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania



**Askofu Amon Kinyunyu**  
Dayosisi ya Dodoma




**Askofu Dkt. Alex Mkumbo**  
Dayosisi ya Kati



**Askofu Michael Adam**  
Dayosisi ya Mkoani Mara



**Askofu Lucas Mbedule**  
Dayosisi ya Kusini Mashariki



**Askofu Dkt. B. Bagonza**  
Dayosisi ya Karagwe



**Askofu Dkt. O. Mdegella**  
Dayosisi ya Iringa



**Askofu Emmanuel  
Makala**  
Dayosisi ya Kusini Mashariki  
ya Ziwa Victoria



**Askofu Andrew Gulle**  
Dayosisi ya Mashariki ya Ziwa  
Victoria




**Askofu Elisa Buberwa**  
Dayosisi ya Kaskazini  
Magharibi



**Askofu Dkt. Steven  
Munga**  
Dayosisi ya Kaskazini  
Mashariki



**Askofu Renard Mtenji**  
Dayosisi ya Ulanga-  
Kilombero



**Askofu Job Mbwiyo**  
Dayosisi ya Kusini  
Magharibi



**Askofu Dkt. Martin Shao**  
Dayosisi ya Kaskazini



**Askofu Charles Mjema**  
Dayosisi ya Pare



**Askofu Levis Sanga**  
Dayosisi ya Kusini Katu



**Askofu Paulo Akyoo**  
Dayosisi ya Meru




**Askofu Dkt. Israel-Peter  
Mwakyolile**  
Dayosisi ya Konde



**Askofu Mameo Ole Paulo**  
Dayosisi ya Morogoro



**Askofu Zebedayo Daudi**  
Dayosisi ya Mbulu



**Askofu Isaya Mengele**  
Dayosisi ya Kusini



**Mchg. Solomon  
Masangwa**  
Kaimu Mkuu,  
Dayosisi Kaskazini Katu



**Bw. Brighton Killewa**  
Katibu Mkuu, KKKT




**Katibu Wakuu**, Dayosisi na KZU, KKKT

## Miaka 50 ya Injili

### Askofu ataka hatua kali zichukuliwe kwa wanaovunja amani

Askofu wa Dayosisi ya Konde ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Israel Peter Mwakyolile (pichani kulia) amevitaka vyombo vya dola vyenye wajibu wa usalama, kulinda watu na mali zao watimize wajibu wao kikamilifu.

Askofu Mwakyolile alisema matukio ya kuchomwa makanisa na uharibifu wa mali za Wakristo yaliyotokea mwaka huu katika maeneo mbalimbali nchini



### Nguvu ya Kristo imeweza kueneza Injili

**Na Askofu Job Mbwiyo  
KKKT Dayosisi ya Kusini  
Magharibi.**

Nachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mungu kwa wale waliotutangulia kuonesha nia ya sisi kuwa wamoja katika kusaidia na kutoa huduma kwa jamii kimwili, kiroho na kiakili. Tunaenzi muungano huu wa miaka 50 ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) uliochukua nafasi mwaka 1963. Tumeona mibaraka mingi katika muungano huu kwa kufanya kazi ya kumtumikia Kristo kwa furaha bila kujali eneo bali katika umoja wetu.

Katika kipindi chote hiki tumeona ufanisi wa kazi ya Mungu umeonekana kwa vitu halisi kama vile kuongezeka kwa idadi ya wakristo wapatao zaidi ya milioni sita ikilinganishwa na wakristo 500,000 mwaka 1963.

Ili kupata watendakazi, Kanisa lili jenga shule na vyuo katika Dayosisi mbalimbali hadi sasa tuna Vyuo Vikuu.

Tumeona watu wengi wanavyojitoa kuendeleza huduma mbalimbali za kiroho na kimwili na hata kupitia urafiki na ushirikiano na makanisa na vyama vya misioni kimataifa. Pia kanisa limefanya kazi katika mataifa mengi kwa ufanisi mkubwa. Yote haya ni matokeo ya uwepo wa kazi zilizoanzishwa na wazee wetu waliotangulia.

Kanisa halitasahau wale wote waliotutangulia kufanya kazi ya Mungu nchini mwetu. Hivyo basi hata sisi tuliofaata tumeendelea kurithi kazi hii ambayo bado tunaendeleza kwa nguvu tunazopewa na Bwana wetu Yesu Kristo. Bado tumeendelea katika nchi yetu kueneza Injili kwa wale wasiomjua Yesu Kristo na hata nchi jirani.

Tumepeleka Injili nchini Kenya, Uganda, Rwanda, Kongo, Zambia, Malawi, Msumbiji, Burundi na nchi nyiningine. Tunawashukuru wenzetu katika nchi hizo waliotupokea kwa

ni viashiria vibaya vya uvunjifu wa amani lakini hakuna kauli wala vitendo vilivyo fanywa na Serikali katika kukemea matukio hayo.

Hata hivyo alisema kuwa Kanisa linasikitishwa na hatua ya Serikali kutochukua hatua kali na za makusudi kukidhibiti wala kukikemea kikundi cha wenyewe msimamo mkali wa dini ambacho kinaonekana kuwa tishio la amani ya Watanzania.


### Nguvu ya Kristo imeweza kueneza Injili

furaha kufanya kazi katika nchi zao. Ni nia ya Kanisa kwetu kuwa kama familia moja inayotumikia Mungu kwa umoja.

Mapokeo ya kuhubiri Injili yalituweke msingi wa kufanya kazi kwa amani, iwe katika familia, vijijini au Serikalini. Amani ilionekana tangu mwanzo na ndio iliyofanikisha kukua kiroho na maendeleo ya kijamii yanayoonekana kila siku. Hata hivyo katika miaka ya hivi karibuni amani imeanza kupungua nguvu zake hata ndani ya kanisa lenyewe kuna uvunjifu wa amani. Kadhalika katika Serikali kuna dalili ya utendaji kazi usioonesha nia ya kudumisha amani iliyokuwepo awali. Hata uhusiano wetu mzuri uliokuwepo kati ya dini na dini unaanza kupotea.

Kusudi la Mungu alilowapa wanadamu ni ili wawewe kuishi kwa amani hapa duniani. Na ndiyo sababu ya kupewa mamlaka ya kutiisha sayari au dunia bila kuiharibu. Ni lengo la maagizo tuliyopewa na Mungu kuitunza dunia. Tunaomba vizazi vinavyokuja viendeleze amani iliyoenziwa na wanafunzi wa Kristo tangu mwanzo hata kama kuna udhaifu unaojitekeza miaka hii ya sasa. Tunaweza kuishinda tukimtegemea Yesu Kristo ambaye tunamtumikia na tutii sauti yake.

Askofu Job Mbwiyo ni Mwenyekiti Halmashauri ya Misioni na Uinjilisti KKKT na ni Mkuu wa KKKT Dayosisi ya Kusini Magharibi yenye makao yake Magoye.



**Askofu Job Mbwiyo  
KKKT Dayosisi ya Kusini Magharibi.**



# Kanisa laahidi kutoa huduma bora

- Hospitali za kanisa hakuna ubaguzi
- Wasio na uwezo ni wengi vijijini

Na Dkt. Geofrey Nimrodi Sigalla

Kikao cha Idara ya Afya ya Kanisa na washirika wake ni mukutano muhimu ambapo kazi za idara zinajadiliwa kwa pamoja katika njia ya uangavu mbele ya wadau husika wanaotoka KKKT, Serikali na nje ya nchi.

Washiriki ni vyama vya misioni, makanisa na taasisi tunazo shirikiana toka nje kama FELM toka Finland, Kanisa la Sweden na DMCDD toka Denmark. Washiriki wengine ni pamoja na Makatibu wa Afya wa Dayosisi, Viongozi wa hospitali zote za KKKT, Wajumbe toka Serikalini (Wizara ya Afya), watumishi wa Vitengo vya Afya KKKT wanao ratibu kazi hizo na wajumbe toka mashirika tunayo shirikiana nayo kama vile Tume ya Kikristo ya Huduma za Jamii (CSS) KKKT inayounganisha makanisa ya Kiprotestanti na Katoliki.

KKKT inatoa umuhimu mkubwa sana kwa kikao hicho cha kila mwaka ambapo

wajumbe wanatakiwa wawe huru kutoa mawazo ya jinsi KKKT inavyoweza kufanya ili kuboresha huduma inazotoa za afya katika vituo vyake.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania lina hospitali 24, zaidi ya vituo 140 vya afya na zahanati na taasisi za mafunzo ya afya. Taasisi na vituo hivi vinatoa huduma za kuzuia maradhi na kutoa tiba. Vituo vingi vya afya vya KKKT viko vijijini kuhudumia watu walio na kipato cha chini katika jamii. Kwa ajili hiyo, ni wazi kwamba si rahisi kupata mapato ya kufidia gharama za uendeshaji kwa uendelevu wa vituo hivi.

Tangu vituo vianzishwe tumekuwa na washirika mbalimbali toka ndani na nje ya Tanzania ambao wamekuwa wakisaidia utoaji wa huduma. Kanisa linapenda kuwashuruku washirika wake wote kwa misaada wanayoendelea kuitoa.

Serikali ya Tanzania imekuwa inatoa fedha za

uendeshaji katika vituo vinavyomilikiwa na mashirika ya dini kwa njia mbalimbali; madawa kwa ajili ya magonjwa kama UKIMWI, kifua kikuu, ukoma na malaria.

Pia serikali inatoa chanjo ili kutoa kinga ya maradhi. Baadhi ya watumishi wanapata ruzuku au kulipiwa mishahara na serikali.

Ni jukumu la serikali kutoa huduma za afya kwa jamii kwa ubia na mashirika ya dini. Tunaisshukuru Serikali kwa kuendelea kutoa mazingira bora ya kutoa huduma za afya. Ni vema iendelee kufadhili utoaji wa huduma katika mashirika ya dini. Pamoja na misaada ya nje na ndani; hospitali za kanisa hasa za vijijini haziwezi kujientesha zenyewe.

Kanisa lina mpango wa kuinua viwango vya zahanati zake ili zikidhi matakwa ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi na Kwamba kanisa linajipanga kutumia teknolojia ili kuinua kiwango cha utoaji huduma za afya kwa Watanzania wote watakahudumiwa katika vituo vyake.



Hospitali ya Haydom ilifunguliwa mwaka 1972 na Mwl. Julius Nyerere. Aliongozana na Dkt. O. Olson (kulia) Mkutugenzi wa kwanza wa Hospitali ya Haydom.

# Kanisa latathmini huduma ya afya

## ● Mchango wa KKKT sekta ya afya

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) linatoa asilimia 15 - 20% ya huduma za afya Tanzania.

Katika sekta ya Afya, Ofisi kuu ya KKKT inajukumu la kuratibu, kuwezesha, kujenga uwezo na kufanya utetezi.

## Serikali yalipongeza Kanisa



*Mwakilishi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jami, Dkt. Elias Kwesi (pichani juu),* alisema Serikali imepongeza Kanisa kwa jithada ya kutoa huduma za hali ya juu katika vituo vyake vya afya nchini Tanzania.

Akifungua mukutano wa kila mwaka wa KKKT na washirika wa sekta ya afya toka ndani na nje ya nchi hivi karibuni, Dkt. Kwesi alisema: "Kupitia sera ya PPP hospitali za KKKT kama Nyakahanga, Bunda na Karatu zimekuwa Hospitali Teule za Wilaya au Halmashauri. Na kwa utaratibu wa Mikataba ya Huduma, Serikali inalipa mishahara, inatoa dawa na kugharamia uendeshaji.


"Sera ya Afya ya Taifa inataka tushirikiane kwa kufanyakazi pamoja na kusaidiana kama ilivyo katika mpango mkakati wa Afya na katika malengo ya milenia.

"Utaratibu wa mikataba ya huduma kati hospitali za taasisi za dini na serikali za mitaa au halmashauri; zimefanya hospitali nyingi kunufaika kama ilivyo kwa hospitali ya KKKT ya Bumbuli iliyopo Lushoto.

"Vituo vya afya vya KKKT viweke kumbukumbu muhimu kurahisisha uingiaji wa mkataba kupitia sera ya PPP.

"Kukabiliana na uhaba wa watendakazi alisema serikali ina mpango wa kupanua vyuo

vyo uganga. Serikali itaangalia namna ya kufadhili vituo maalum kama Lutindi kupitia Wizara ya Afya moja kwa moja."



*Askofu Paulo Akyoo, Mkuu wa Dayosisi ya Meru (pichani juu),* alisema safari ya Mpango wa Afya Endelevu KKKT ni ndefu lakini yenye mafanikio kwa kufanya kazi pamoja na Serikali, washirika wa nje, ndani kama vile CSSC.

Baada ya ripoti ya tathmini kutolewa washiriki wa mukutano walishukuru kupokea taarifa hiyo na kusifu mafanikio ya Programu ya KKKT ya Afya Endelevu. Kipekee shukrani zilitolewa kwa waratibu wa vitengo vya KKKT vya Afya na Ofisi Kuu kwa kusimamia Progamu kwa ufanisi. Pamoja na mafanikio, vituo vya afya vimekuwa na changamoto kama uhaba wa watendakazi; kutokuwa na mikataba ya huduma kwa baadhi ya vituo vya mashirika ya dini na Serikali; uhaba wa rasilimali ili kutekeleza sera ya afya; na kukosekana kwa mfumo wa kusaidia vituo maalumu kama vile Lutindi Wilayani Korogwe. Washiriki wa mukutano walitaka watekelezaji waweke maanani uendelevu wa huduma bora kwa kutafuta vyanzo mbadala vya mapato ili kuendelea kutangaza upendo wa Mungu.



## Katibu Mkuu ashukuru Serikali

Katibu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Bw. Brighton Killewa, (pichani juu) akiongea wakati wa ufunguzi wa kikao cha washirika (partners) wa KKKT katika sekta ya afya kilichofanyika Arusha hivi karibuni. Pamoja na kusema mambo mengine aliipongeza Serikali na

washirika wote wa sekta hii kwa misaada inayowezesha Kanisa kutoa huduma za tiba katika hospitali zake.

Kikao hicho pia kilijadili ripoti ya Tathmini ya Mpango wa KKKT wa Huduma ya Afya Endelevu (*ELCT Managed Health Care Programme*).

## Mpango wa Afya Endelevu KKKT

Mpango wa Afya Endelevu wa KKKT uliridhiwa na Halmashauri Kuu ya Kanisa mwaka 1994 kwa lengo la kuinua kiwango cha ubora wa huduma katika vituo vya afya vya KKKT.

Awamu ya kwanza ilikuwa 1997 - 2002; Awamu ya pili ilikuwa 2003 - 2007; tathmini ilifanyika 2006.

Awamu ya tatu ilikuwa 2008 - 2012. Baada ya awamu hiyo ndipo tathmini ilifanyika.



Dkt. Geofrey Sigalla  
Mkurugenzi wa Afya KKKT.



# Kupunguza Umaskini

## Kanisa ni mdau wa maendeleo



Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) pamoja na kueneza Neno la Mungu, wakati wote limefanya kazi kwa karibu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wadau wengine katika kujengea uwezo jamii ya Kitanzania kwa kuibua na kutekeleza miradi/programu mbalimbali za maendeleo.

Malengo ya Programu/ miradi hiyo ni kupunguza umaskini, upungufu (uhaba) wa chakula, magonjwa

(maradhi) na kufuta ujinga mionganoni mwa jamii katika eneo linamofanya kazi.

Mradi wa Ng'ombe wa Maziwa (*Dairy Cattle Farming Project*) ulianzishwa mwaka 1984 ili kupunguza umaskini.

Kupitia mradi huu Kanisa limekuwa likigawa mitamba wenye mimba kwa watu wenye kipato duni, wajane na wagane, walemaru, yatima, wanawake na watu wanaoishi na VVU bila kujali dini, dhehebu wala kabilo.

## Lengo kuu la mradi

Lengo la kuwagawia walengwa mitamba ni ili wawze kutumia ng'ombe wa maziwa kuboresha afya zao kwa kunywa maziwa, kuongeza uzalishaji katika kilimo kwa kutumia samadi ya ng'ombe, kuongeza kipato kutokana na mauzo ya maziwa na ndama/ ng'ombe wa ziada. Mradi huu ulifika kikomo Juni 2010 ukiwa tayari umegawa mitamba

1,520 na madume 150 katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Kutohana na kupeana ndama wa kwanza jike wananchi zaidi ya 7,000 wamefikiwa na mradi huu. Pamoja na ugawaji wa mitamba na ndama mradi ulielimisha jamii katika utunzaji wa mazingira, uundaji na uendeshaji vikundi, ujasiriamali, jinsia na maendeleo na UKIMWI.



Programu ikishiriki katika maonyesho ya siku ya Mazingira duniani iliyofanyika kitaifa mjini Moshi mwaka 2012.

## Jamii yanufaika

Utekelezaji wa mradi huu umeimarisha upendo na mshikamano mionganoni mwa jamii sio tu kati ya wale wanufaika bali katika maeneo husika. Familia nyingi zimeongeza kipato kutokana na uuzaaji wa maziwa ya ziada na ng'ombe wanaozaliwa baada ya kutoa ndama wa kupeana na yule wa kurudisha

kwenye mradi.

Kuongezeka kwa mapato kumeziwezesha familia zilizonufaika na mradi kutekeleza mambo mbalimbali ya kimaendeleo kama kununua mashamba, kununua viwanja na kujenga nyumba bora, kulipa ada kwa ajili ya masomo sekondari na vyuo.



*Askofu Anders Wejryd,  
Askofu Mkuu wa Kanisa  
la Sweden, akizungumza  
na Bibi Yokonia Enoch  
Pallangyo, nyumbani kwake  
Nkoaranga. Bibi huyu ni  
mionganoni mwa wafugaji  
waliopokea mtamba kutoka  
Mradi wa Ng'ombe wa  
Maziwa KKKT mwaka 2004.  
Baada ya kupokea mtamba  
sasa anaweza kutunza  
wajukuu waliochwa yatima  
baada ya mtoto wake na  
mkewe kufariki.  
Mmojawapo wa wajukuu  
amekaa chini nyuma ya  
askofu. Kulia ni mratibu  
wa Mradi, Bibi Patricia  
Mwakikenda.*



*Watumishi wa Mradi wakiwa na viongozi wa kampuni ya ujenzi wa mitambo ya biogesi toka Dayosisi za Meru na Dayosisi ya Kaskazini waliofika Ofisi Kuu ya KKKT tarehe 03 Juni 2013 kuhamasisha utunzaji wa mazingira. (c) 2013 KKKT.*

## Utunzaji mazingira

### Inatoka uk 13

Pia kutokana na kuongezeka kwa kipato biashara ndogondogo kama vioski

ya chakula, maduka madogo kwa ajili ya kuuza bidhaa ndogondogo, maduka ya ushonaji zimeanzishwa na kuendeshwa na wanufaika wa mradi. Hii imeongeza mapato zaidi kwa familia hizo.

Katika kutekeleza mradi huu

kipaumbele mojawapo kimekuwa ni utunzaji wa mazingira. Ili kutekeleza azma hii wanajamii wamefundishwa na sasa wanalima kilimo bora kinachozingatia utunzaji mazingira kama kilimo cha makingo, kilimo hai, bustani ya jikoni, matuta ya kina kirefu na utengenezaji wa mboji kwa kutumia masalia mbalimbali. Upandaji miti malisho na upandaji wa miti ya matunda na mbao katika maeneo yao.

### UTENGENEZAJI MBOJI




*Mafunzo kwa viongozi wa Eneo la Misioni Rukwa KKKT, Serikali za Mitaa, Washarika na wawakilishi wa wananchi wakiwa katika semina iliyofanyika Mpanda hivi karibuni, wakipata maeleo juu ya uendeshaji wa Programu ya Uhai na Mazingira kwa kuzingatia haki na usawa.*



*Wafugaji wa Jimbo la Chalinze, Dayosisi ya Morogoro, wanufaika na mafunzo ya utengenezaji wa mboji ili kuepuka matumizi ya mbole za viwandani ambazo ni za gharama kubwa na vigumu kupatikana; lakini pia zinaharibu mazingira kwa kusambaza sumu ardhini.*

# Utoaji wetu kwa ajili ya kazi za Umoja KKKT



**Askofu Elisa Buberwa,  
Dayosisi ya Kaskazini Magharibi.**

Juni 23, 2013 ni siku ya kilele cha maadhimisho ya Jubilii ya miaka 50 ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Kazi moja wapo katika maadhimisho hayo ni kujikumbusha matendo mbalimbali yaliyotusaidia kurutubisha umoja wetu ambao ni tunu muhimu katika maisha yetu kama Kanisa la Kilutheri nchini. Moja wapo ya matendo hayo ni utoaji wetu (dayosisi na vituo vya Kanisa) kwa ajili ya **Kazi za Umoja (KZU)**. Katika makala haya mafupi nitajadili kuhusu utoaji wetu na umuhimu wake katika kuimarishe KZU na hivyo kuimarishe umoja wetu tukiwa Kanisa moja, KKKT.

Kwanza tunatoa shukrani nyingi kwa Mungu aliyetuunganisha na sasa anaendelea kutuwezesha kukua katika muungano huu. Kama taifa vile, mwaka 1963 tulikuwa wachanga sana - mwaka wa pili baada ya uhuru. Tumekua katika maeneo mengi ya maisha yetu – imani, theologia, ufanamu, upeo, idadi ya wakristo, huduma, uchumi, idadi ya dayosisi/ vituo, ushawishi, n.k.

**Kazi zetu za Umoja** ziko katika maeneo haya: Ofisi Kuu - Arusha, mikutano, elimu, afya, diakonia, mipango na maendeleo; mahusiano yetu na makanisa, serikali, mashirika ya kitaifa na kimataifa. Ni kazi nyingi na zinatumia gherama kubwa.

Gherama hizi, kimsingi, huchangiwa nasi wana KKKT. Ni kweli kwamba marafiki (partners) zetu hutusaidia, na pengine kwa kiasi kikubwa cha fedha na vitendea kazi, lakini tunajua kuwa ni jukumu letu sisi sote kuzigharamia. Kazi hii tumeifanya kwa takribani miaka 50 iliopita. Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya wakristo na watu wengine waliochangia na wanaochangia juhudi hizi.

Tunafahamu kuwa umoja wowote wa kweli huanzia moyoni. Kupenda umoja ni msingi wa kutenda majukumu yanayodaiwa na umoja huo. Wakristo wa kanisa la kwanza tunaambiwa walipenda umoja kutoka moyoni:

*“Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu chochote alichochote nacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika”* (Mdo. 4: 32). Ni kweli, kwamba hiki ni kiwango cha juu kabisa cha umoja, ijapokuwa, baadaye, baadhi ya wanafunzi walishindwa kutekeleza makubaliano hayo; lakini kitendo chao cha kumiliki mali kwa pamoa ni kielelezo kizuri kwa ajili yetu kujifunza jambo la umoja kivitendo.

Katika suala zima la umoja, kuna mambo mawili:

- (a) Makubaliano.
- (b) Utii.

Katika KKKT, mathalan, tumekubaliana kuwa tutachangia kazi zetu za umoja kwa njia ya:

- (a) Asilimia mbili (2%) ya matoleo yetu ya kila mwezi, dayosisi zote ziyatume Makao Makuu, Arusha.
- (b) Matoleo ya sadaka (yote) ya Sikukuu ya KKKT, kila mwaka yatumwe pia Makao Makuu.
- (c) Michango wa Misioni nchi za jirani, kipo kiwango maalum kwa kila dayosisi.
- (d) Michango mingine ya msimu, kama michango wa Jubilii ya miaka 50, KKKT.

Kikristo na hata kiungwana, baada ya kufanya makubaliano ni muhimu sana kuyatii, tena, kwa uaminifu. Kwa ngazi ya usharika, tukikubaliana kuchangia kazi fulani kwa njia ya mitaa ya usharika, basi mitaa ifanye hivyo kwa uaminifu; kadhalika kwa ngazi ya jimbo,

dayosisi na kanisa zima ambapo dayosisi zote zinawajibika kutii makubaliano ya pamoa.

Jambo la uaminifu ni kubwa kwani Kanisa linatazamiwa kuwa mwalimu wa uaminifu kwa jamii inayolizunguka. Ikiwa, kwa mfano, uongozi wa mtaa fulani hauzingatii uaminifu katika makusanyo na mawasilisho ya sadaka yote ya **Sikukuu ya KKKT**; wakristo mtaani humo watakuwa wamepotoshwa na uongozi huo katika habari ya uaminifu kuhusu maamuzi yetu wenye. Hivyo hivyo, ngazi ya Usharika, Jimbo, Dayosisi na KKKT nzima – tunatakiwa kuwa vielelezo – maisha ya mfano mzuri wa kuigwa.

Jambo hili ni changamoto kwetu sote. Zipo dayosisi zinazofanya vizuri katika kuwasilisha michango Makao Makuu, Arusha; na nyingine hazifanyi vizuri. Wito wa viongozi wetu, mara kwa mara ni kuwa sote, ngazi zote, tujitahidi kutimiza jukumu hili bila shuruti.

Ndugu Barnaba, mmoja wa wanafunzi wa Bwana Yesu alijipatia sifa njema kwa kutii, tena kwa uaminifu, makubaliano ya jamii ya watu walioamini. Yeye

**“Jambo la uaminifu ni kubwa kwani Kanisa linatazamiwa kuwa mwalimu wa uaminifu kwa jamii inayolizunguka – Askofu Buberwa”**

aliuza shamba lake, na kukabidhi fedha yote kwa mitume (Mdo. 4: 37). Barnaba anaelezwa kuwa alikuwa mtu mwema, mwenye imani, ameaja Roho Mtakatifu na mwenye ushuhuda mzuri (Mdo. 11: 24). Ninaamini, siri ya utii na uaminifu iko pale!

Tunapoahimisha miaka 50 ya umoja wetu katika KKKT, tumwombe Bwana atujalie sifa kama walizokupa nazo watangulizi wetu akina Baranaba na wenzake wengine. Katiba ya mwanzo kabisa ya KKKT ina maneno: **“Tulishirikiana pamoja katika kazi za umoja, kwa njia ya Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Tanganyika,...”** (Katiba KKKT, Tololo 2007 ukurasa iv).

Basi na sisi tuendelee kushirikiana katika kazi za umoja na Bwana atubariki katika miaka 50 ijayo.



# Injili yaenea Mtwara na Lindi

*Na Askofu Lucas Mbedule  
KKKT Dayosisi ya Kusini Mashariki*

Kanisa la kilutheri lilifungua huduma ya Injili Eneo la Mtwara na Lindi kwa mara ya kwanza mwaka 1964 chini ya Sinodi ya Uzaramo/Uruguru kwa kumtuma Mtumishi aliyeitwa Petro Eliya, huyu alifanya kazi pale Lindi tangu 1964 Januari na aliondoka ghafla mwishoni mwa mwaka huo 1964.

Huduma ikasimama hadi 1 Tarehe Aprili 1968 kazi ya kutunza Eneo hili ilikabidhiwa kwa Sinodi ya Kusini wakati huo, ambayo sasa ni Dayosisi ya Kusini.

Tarehe 1 April 1969 - 1973 Shemasi Gerson Mng'ong'o anatumwa kuanza kazi Mtwara. Na mionganini mwa Wakristo wa kwanza eneo hili Miaka ya 1970 ni Bw. Invocavit Mushi – Yupo hadi sasa ni Mwinjilisti wa kujitolea, Marehemu Dkt. Kleruu akiwa Mkuu wa Mkaoa wakati huo na Ndugu Mwaipopo - alikuwa Mkuu wa Gereza la Rilungu Mhe. Jaji Robert Kisanga - Jaji Mstaafu hao ndio waliosaidia hadi kupatikana kiwanja kwa ajili ya kazi ya Bwana.

Mwaka 1970 Kanisa linaanza kujengwa, na mwaka 1975 Ujenzi unakamilika mwaka 1975 na mtu wa kwanza mwenyeji, alipokea Ukristo (Emmanuel Mpunga) toka kabilila la Wamwela-Ruangwa.

Mwaka 1973 - 1977 Mchungaji wa pili alitumwa kufungua Usharika wa Lindi (Mchg. Cleopa Lukilo sasa ni Askofu Mstaafu). Mwaka 1973 kazi ya Injili ilifunguliwa Masasi na Mwj. Gideon Mwambyale alitumwa kwa mara ya kwanza. Na Mchungaji Emmanuel Nyang'uye alikuwa Mchungaji wa kwanza Masasi. Mwaka 1975 Kanisa lilifungua huduma huko Nachingwea. Huduma za Sakramenti

zilitunzwa na Usharika wa Lindi. Mwaka 1982 Kanisa likakamilika kujengwa.

Mwaka 2001 Kanisa liliwekwa wakfu na Mkuu wa Kanisa kwa wakati huo, Mhe. Askofu Dkt. Samson Mushemba. Mwaka 1971 Stesheni ya Newala ikafunguliwa na Mwj. Lameck Masawa akawa mtumishi wa kwanza. Mchg Anton Mabena alitumwa kwa mara ya kwanza mwaka 1981 – 1985.

Mwaka 1998 Eneo la Missioni la Mtwara/ Lindi likafanywa Jimbo.

Mwaka 1998 – 2002 SEM (Swedish Evangelical Mission) ikamtuma Mchg. Ingemar Holmequist kuwa Mmisionari. Mwaka 1998 – 2005 Mchungaji Daniel Mbembati akawa Mkuu wa Jimbo vipindi viwili. Mwaka 2005 – 2013 Mchungaji Lucas Mbedule akawa Mkuu wa Jimbo vipindi viwili.

Mwaka 2005 maandalio ya Dayosisi

yalianza. Mwezi Machi 2006 Kamati ya Katiba ikaundwa. Mwaka 2007-2009 wanafunzi wa kwanza wa Uchungaji wakahitim. Mwaka 2008 Sharika mpya zikafunguliwa Kilwa, Liwale, Ruangwa na Tandahimba. Mwaka 2010 kazi ya kugawa ramani ya Dayosisi ikafanyika. Mwaka 2011 kazi ya kuandaa ikaendelea na vikao vya Dayosisi ya Kusini (DKU) na KKKT viliendelea kupitia taarifa mbalimbali.

April 2012 Halmashauri Kuu ya DKU ikatoa kibali kuwa tangu Septemba Jimbo lianzu kuitwa '**Eneo Maalumu linaloandaliwa Kuwa Dayosisi'** na kuwa Kiongozi wake aitwe **Mkuu wa Eneo.**

Tarehe 18 Desemba 2012, Sharika nyingine zikafunguliwa Mangaka, Ndanda, Hingawali, na Somanga. Mwezi Agosti 2013 Mkutano Mkuu wa kwanza wa Eneo ulikaa na kupitisha Rasimu ya Katiba na Miongozo ya Dayosisi. Tarehe 14 Desemba 2012 Mkutano Mkuu Maalumu wa Uchaguzi wa Askofu na Msaidizi wa Askofu ulifanyikia Masasi. Mchg. Lucas Mbedule alichaguliwa kuwa Askofu.

Jumlisho

Dayosisi hii imeanza ikiwa na Majimbo 6; Sharika 14; Mitaa 52; Wachungaji 15; Wainjilisti 34 na Wazee wa Kanisa 156.

Hivyo basi kama alama ya kuzaliwa kwa Dayosisi hii, Halmashauri Kuu imeamua kuwa ujengwe mnara utakao wakumbusha wakristo siku zote kuwa '**Mungu wetu wa Utatu' hataliacha Kanisa lake pekee yake wakati wote;** Mnara huu unaonyesha alama ya '**Utatu wa Mungu'** na kuwa Dayosisi hii imezaliwa '**Siku ya Utatu' na itajengwa katika mafundisho ya Utatu Mtakatifu.**



Tarehe 26 Mei ilikuwa ni shangwe katika Kanisa Kuu la Kilutheri Mtwara Askofu Lucas Mbedule (mwenye fimbo) alipowekwa wakfu kuongoza KKKT Dayosisi ya Kusini Mashariki. Picha ya pamoja Waziri Mkuu Mizengo Peter Pinda (katikati) akiwa na Askofu na msaidizi wake na wenzi wao. Kushoto ni Mkuu wa KKKT na nyuma ni Wamisionari walioshiriki Ibada. (PICA © 2013 KKKT)

# Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira

Kutoka seminari ya kilutheri hadi kuwa Chuo Kikuu

MIAKA  
50  
KKKT



Uongozi mpya wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira. Safu ya mbele kutoka kushoto ni Profesa Joseph Parsalaw Makamu Mkoo wa Chuo; Profesa Esther Mwaikambo Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo, Askofu Dkt. Alex Malasusa Mkoo wa Chuo na Mkoo wa KKKT, Profesa John Shayo Makamu Mkoo wa Chuo aliyeondoka na Bw. Brighton Killewa mjumbe wa bodi na Katibu Mkoo wa KKKT.

## Seminari ya Kilutheri ilivyoanza


Na Profesa Joseph Parsalaw  
**Makamu Mkoo wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira**

Historia ya Seminari ya Kilutheri ya Makumira huanzia mwaka 1947 wakati Makanisa ya Kilutheri hapa nchini yakiwa chini ya Vyama vya Misioni. Makanisa haya yalikubaliana kuunganisha nguvu zao ili watheologia (Wachungaji) waandaliwe kwa pamoja


katika msingi na mafundisho sahihi ya Kilutheri kwa kuzingatia mtaala wa pamoja.

Kabla ya uamuzi huu wa kuwaandaa watumishi kwa pamoja, kila Kanisa la Kilutheri nchini lilijiandalia watumishi wake. Mnamo mwaka 1947 huko

Lwandai kwenye miteremko ya milima ya Usambara, Chuo cha Kuelimisha Wachungaji kilianza kwa kuwasomesha wanafunzi wa kwanza 58 katika kozi ya theology iliyodumu kwa miaka 3 na kuhitimu baada ya miaka mitatu tarehe 14/10/1949. Wanafunzi hawa wa theology wa kwanza waanzilishi wa Lwandai walitoka sehemu mbalimbali ya Tanzania. Kwa heshima yao kama waanzilishi orodha yao ni kama ilivyo ukurasa unaofuata ikionyesha jina na Usharika aliotoka.



MAKTABA YA CHUO



Madarasa ya theology ambayo baadhi yametumika tangu 1954 chuo kilipohama toka Luandai, Lushoto na kuhamia Makumira.

# Wanafunzi 58 wa kwanza Lwandai

**Yafuatayo ni majina ya wanafunzi waanzilishi wa Lwandai na mahali atokako katika mabano:**

1. Abraham Ng. Msumri Msongolo (Funta)
2. Aletaulwa Nkini (Shira)
3. Ananidze Lutengamaso Bange (Illembula)
4. Andrea Mwakamsale (Manow)
5. Andrea Mwilukisaulo (Kigarama)
6. Andolye Lugano Mahenge (Bulongwa)
7. Asombwile Mwalukasa (Mwakaleli)
8. I. Athanasio Kabelinde (Lwantage)
9. K. Anaeli Abrahamu Macha (Mbokomu)
10. Bartimayo Mnkama (Tanga – Mashamba)
11. Christian Mushumbusi (Kyamutwala)
12. Clement Kingu (Ihanja)
13. Daniel Kimbwereza (Mbaga)
14. Eliezer Kelefu (Tewe)
15. Elinisafi Mapunjio (Vudee)
16. Elinsa Kisaka (Old-Moshi)
17. Elyahu Meiliari (Ilboru)
18. K. Ehraim Amos (Marangu)
19. Ernest Kalembo (Kashasha – Misenyi)
20. Ezekiel S. Mpumilwa (Bulongwa)
21. Filemon Daffa (Mponde)
22. Filipo P. Njuga Daffa (Ngwelio)
23. Huruma Filemoni Mdheru (Maneromango)
24. Jeson Ruben Chando (Dar es Salaam)
25. John Lytakayamilwa (Ibwera)
26. Jonathan M. Kitalama (Wilwana)
27. Kornelio Jairo Kimaro (Masama)
28. Kristiani L. Lutahakana (Kanyangereko)
29. Kundaeli Muro Nkyia (Masama)
30. Leonard L. Lubago (Bugabo)
31. Loibooki Tomitho (Kimandolu)
32. Lunogelo Mgengaungu Kinyamagoha (Isimikinyi)
33. Manase M. Yona (Kiomboi)

34. Matia B. Lutosha (Ndolage)
35. G. Mattayo Samweli (Ushora)
36. Mhando Mbughuni (Ngulwi-Lushoto)
37. Mikaeli Yohana Mhombo (Bungu)
38. Moses Marko Kaniki (Kwengiti)
39. Naftali Lomani (Arusha)
40. Nathanaeli Jeremiah Ngowi (Mwika)
41. Ndelilio Tadayo Palangyo (Nkoaranga)
42. Ojungu Meshwareki (Olboru)
43. Paulo Mkali (Isanzu)
44. Petro Sh. Aron (Kinampanda)
45. Samwel P. Semeji (Mlalo)
46. Sifigate Lusanjala Luvanda (Magoye)
47. M. Simeon K. Petro (Lambi)
48. Stefano Reuben Moshi (Mamba)
49. Stefano Kaaya (Nkoaranga)
50. Teofilo Balige (Lwantege)
51. Yeremia Njeta Kaaya (Nkoaranga)
52. Yessaya P. Mshihili (Mtae)
53. Yohana Kusaga (Mlalo)
54. Yohana Msigwa (Kidugala)
55. T. Yoonazi Kikujji (Gonja)
56. Yosefu Kiwope (Pommerin)
57. Ndesanjo Ngilekiro Mfurru (Marangu)
58. A. Ndesangio Ndesamburo (Masama)

Hao ndio wanafunzi waanzilishi wa Chuo cha Theologia cha Lwandai.

## WAALIMU

Walimu waliofundisha darasa hili la kwanza ni Mch. Dk. Daniel Frieberg aliyekuwa Mkuu wa Chuo na Mch. Herbert Uhlin na mwenyeji aliyeitwa Bwana Filipo Njau. Darasa la pili lilifuata mwaka 1950 – 1952 lilikuwa na wanafunzi 25. Mkuu wa Chuo alikuwa Mch. Herbert Uhlin na Mchungaji mwenyeji Ephraim K. Amos na darasa hili lilihitimu Oktoba 1952.



## Sababu za kukua eneo la Makumira

Chuo cha Lwandai kilihamishiwa hapa kilipo sasa Makumira mwaka 1954.

Sababu kubwa ya Kanisa kuamua kuhamishia Chuo hapa Makumira ni ukubwa na eneo. Eneo hili la Makumira lilikuwa shamba kubwa la kahawa ambalo lilifaasana kwa upanuzi wa Chuo ukilinganisha na eneo la Lwandai ambalo ni dogo kwa upanuzi wa Chuo. Kigezo cha pili ni mahali Makumira ilipo, pembezoni kabisa mwa barabara itokayo mjini Arusha kwenda Moshi na kwingineko.

Makumira ni eneo ambalo liko ndani ya Dayosisi ya Meru ya Kanisa la Kiunjili la Kilutheri Tanzania. Mtu mgeni ajapo kutembelea Makumira atakaribishwa na mandhari nzuri ya miti mikubwa mingine yaweza kuwa na umri wa karibu miaka mia moja na zaidi. Miti hii mikubwa inaendelea kubeba historia ya shamba la Makumira lililoanzishwa miaka ya 1905 na Mmisionari Bwana shamba Albert Fokken na Uffe Fokken kutoka Chama cha Missioni ya Leipzig, ambao ndio walioanzisha Ulutheri sehemu hii ya kaskazini mwa nchi ya Tanzania.

Chuo hiki cha Wachungaji kama kinavyofahamika kwa watu wengi kilifunguliwa rasmi hapa Makumira tarehe 29/08/1954.

*Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira waliohitimu mwaka 2012 wakifurahi walipopata nafasi ya kupiga picha na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Askofu Dkt. Alex Malasusa ambaye pia ni Mkuu wa Kanisa la Kiunjili la Kilutheri Tanzania.*



*Juu ni jengo la Utawala la Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira. Chini ni majengo ya Kitivo cha Sayansi Jamii, Sheria na Elimu.*

Chuo hiki kilanza kwa kufundisha Wachungaji kwa Kozi ya Cheti na darasa la kwanza kwa hapa Makumira lilanza na wanafunzi 44 wakitokea sehemu mbalimbali ya nchi yetu. Kwa muda mrefu wito wa kusomea huduma hii ya kueneza Neno la Mungu ilikuwa kwa wanaume tu hadi miaka ya baadaye wanawake walipoanza kujiunga na masomo ya theologia. Kozi ya cheti cha theologia iliendelea hadi 1962. Na kuanzia mwaka huo Kozi ya Stashahada ya theologia ilianzishwa. Wakati huo kozi hii ilifundishwa kwa ushirikiano wa Idara ya Mafunzo ya Dini ya Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda. Mwaka 1974 Kozi ya Shahada ya Kwanza ya Theologia

ikaanzishwa na mwaka 1980 Kozi ya Stashahada ya Theologia ikasitishwa.

Mwaka 1996 Halmashauri Kuu ya Kanisa kwa kuzingatia kukua kwa Chuo cha Makumira ikaridhia Chuo cha Makumira kiundwe kwa mfumo wa kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini. Uamuzi huu wa Halmashauri Kuu ulikubali pia kuongezwa kwa vitivo vingine. Mwaka 1997 Makumira ikawa Chuo Kikuu Kishiriki na mwaka huo kukaanzishwa Shahada ya uzamili ya Theologia. Mwaka 2004 kwa kushirikiana na Vyuo Vikuu vya nje na ndani ikaanzishwa kozi ya shahada ya uzamivu.

Chuo Kikuu Kishiriki cha Makumira kilipandishwa hadhi na kuwa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira tangu tarehe 5/8/2011. Badiliko hili la kuwa



*Picha ya pamoja ya wajumbe wa Halmashauri Kuu ya KKKT ambayo ilikutana hivi karibuni. Halmashauri Kuu ni kikao cha maamuzi cha ngazi ya juu baada ya Mkutano Mkuu .*

Chuo Kikuu kinachojitegema lilitokana na uamuzi wa Halmashauri Kuu ya Kanisa. Ni pamoja na Vyuo Vikuu Vishiriki vya KCMUCo, Moshi IUCo, na SEKUCo vikaruhusiwa kujiandaa kuwa Vyuo Vikuu vinavyojitegemea. Hadi sasa ni SEKUCo tu kilichofanikiwa kuwa Chuo Kikuu kinachojitegemea na vingine bado vinaendelea na mchakato hadi kukidhi vigezo vya Baraza la

Ithibati la Taifa (TCU).

Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira kina Vitivo vya Theologia, Sayansi ya Jamii, Kitivo cha Sheria, Kitivo cha Elimu na Kitivo cha Sayansi.

Kozi mbalimbali zinazotolewa katika Vitivo nilivyovitaja vitaweweza kuonekana katika Tovuti ya Chuo: [www.makumira.ac.tz](http://www.makumira.ac.tz) na katika Prospectus ya Chuo mwaka 2012-2015 uk. wa v – vii.

# Vyuo Vikuu vishiriki

Chuo Kikuu cha Tumaini kilanzishwa 1997 na Makamu Mkoo wa kwanza akiwa Prof. John Shao na Makao Makuu yakiwa Moshi hadi kilipohamia Makumira tarehe 24/09/2009. Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira kina Vyuo Vikuu vishiriki vifuatavyo:-

- Chuo Kikuu Kishiriki Iringa.
- Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba cha KCMC.
- Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini Makumira Dar es Salaam.
- Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu Stefano, Moshi.



Maktaba ya kisasa ya teknolojia na hali ya juu ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Iringa.



Uongozi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Josia Kibira.



Mkoo wa KKKT ambaye pia ni Mkoo wa Chuo Kikuu cha Tumaini akizindua madarasa ya kampasi ya Mwenge ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam (TUDARCO).



Picha ya maktaba ya wahitimu wa Chuo Kikuu Kishiriki -KCMC.

## Wakuu wa Chuo cha Makumira

Mkoo wa Chuo wa kwanza kikiwa Lwandai ni Mch. Daniel Frieberg ambaye alifuatiwa na Mch. Herbert Uhlin mwaka 1950 hadi kustaafu kwake 1961. Alifuatiwa na Mch. Eliewaha E. Mshana na kuongoza Chuo hadi 1972 isipokuwa kati ya 1965 – 1966 Mch. Dk. Howard S. Olson alishika uongozi. Mch. Thomas Musa akawa Mkoo wa Chuo kwa miaka miwili 1973 – 1974. Mch. Dk. Sebastian Lutahoire akachukua uongozi kuanzia 1975 hadi Mei 1980. Kuanzia Januari 1980 hadi Aprili 1980 Mch. Siprian Yakobo akawekwa kuwa "Mwangalizi" wa Chuo.

Mch. Dk. Oriville Nyblade akachaguliwa kuwa Mkoo wa Chuo kuanzia Aprili 1980 hadi Juni 1984. Mch. Dk. Hance A. O. Mwakabana akawa Mkoo wa Chuo kuanzia 1984 hadi Mei 1992. Mch. Dk. Wilson B. Niwigila akafuatia kuwa Mkoo wa Chuo kuanzia Julai 1992 hadi Novemba 1998. Mch. Prof Dk. Gwakisa E. Mwakagali alifuatiwa kuwa Mkoo wa Chuo Januari 1999 hadi Mei 2007. Mch. Prof. Dk. Joseph W. Parsalaw akafuatia kuwa Makamu Mkoo wa Chuo kuanzia Mei 2007 hadi 4/8/2011. Baada ya mchakato wa Makumira kupata hadhi ya Chuo Kikuu kinachojitegemea, Mch. Prof. Dk. Joseph W. Parsalaw akachaguliwa kuwa Makamu Mkoo wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA) tangu 5/8/2011 hadi sasa.


- Chuo Kikuu cha Josia Kibira na
- Kituo cha Tumaini Makumira Mbeya (SHUCO). Ninapenda kumalizia mwendo mzima wa kuanzishwa na kukua kwa Chuo kikiwa Chuo cha Theologia hadi sasa kikiwa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira kwa kunukuu kutoka Zaburi 103:1-2

"Ee nafsi yangu umhimidi BWANA. Naam, vyote vilivyo ndani yangu vilihimidi jina lake takatifu. Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA, wala usizisahau fadhili zake zote."




Makamu Mkoo wa Chuo Kishiriki cha Kumbukumbu ya Stefano Moshi (SMMUCO) (wa kwanza kulia) akipokea vitabu kwa ajili ya maktaba ya chuo.

# Waasisi walitaka twende pamoja kwa umoja



Askofu Dkt. Alex Malasusa, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania tangu 2007.



Askofu (Mstaafu) Dkt. Samson Mushemba, Mkuu wa Tatu wa KKKT 1992 - 2007.



Marehemu Askofu Dkt. Stefano Moshi, Mkuu wa 1 wa KKKT, 1963 - 1979.

Wenye busara wa dunia hii hutukumbusha kwa kusema umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Akifunga kikao cha hivi karibuni cha Halmashauri Kuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dkt. Alex Malasusa, alisema: "Tudumishe mazuri tuliyojiweke na miyo inapoguswa kwa jambo linalohamasisha utendaji tutende. Alisema nguvu tulionyayo kama Kanisa ni kutokana na umoja wetu.

"Tumerithi hatua za watu (yaani waanzilishi wa KKKT) waliokuwa na msimamo wa kutaka **kwenda pamoja kwa umoja**. Tuombe Mungu atuondolee ubinaksi na apandikize umoja.

"Ukimwekea Mungu nadhiri usikawie kuiondoa. Ni afadhalini

usiweke nadhiri kuliko kuweka kisha usiiondoe. Tuondoe nadhiri tunapoweka wala tusibaki kama wale wanawake wapumbavu ambao hawakuiandaa kumlaki bwana harusi bali tuige mfano wa wanawake wenye busara waliokuwa wamejaza taa zao mafuta wakisubiri kumlaki bwana harusi.

"Sisi (viongozi ndio) wenye zamu hivyo tulitumikie Kanisa tukijua hii ndio zamu yetu. Kwa mfano tukishindwa kuimarisha mazuri tulionyayo, tusipotoa mafundisho **Shule za Jumapili** au tusipoweka nidhamu katika shule, vyuo hasa vya kutoa elimu ya theolojia; tujue ni katika zamu yetu tumeshindwa." Alisema.

## Vyama hivi vitatu vilieneza Ulutheri

Na Mchg. Profesa Joseph Parsalaw



Mwanzo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika (baadaye Tanzania) kuwepo nchini ni mwaka 1887, Chama cha Misioni cha Berlin III au Evangelical Missionary Society for East Africa (EMS) kutoka Ujerumani kilipoanzisha kazi ya Injili pale Dar es Salaam.

Chama cha pili, Chama cha Misioni cha Berlin I, nacho kutoka Ujerumani, kiliingia Tanzania kikitokea Afrika ya Kusini na kuanza kazi Nyanda za Juu Kusini mwaka 1891 kilipoanzisha kituo au misheni sehemu iitwayo Ipagika au Pipagika (Wangemannshöhe) katika Dayosisi ya Konde.

Mnano mwaka 1890 Chama cha Berlin III kilibadilika kufuatana na haja iliyokuwepo na kikachukua sura mpya baada ya kubadili sera yake na kujulikana kwa jina la Bethel au Misioni ya Bethel. Misioni hii ikafika sehemu za Tanga na kuanza kazi sehemu ijlukanayo kwa jina la Mbuyukenda

B a a d a y e Misioni hii iliamua kufikisha Injili ya Kristo nje ya mipaka ya Tanganyika, wakaamua kwenda Rwanda. Ili kufika Rwanda,



Marehemu Askofu Dkt. Sebastian Kolowa, Mkuu wa Pili wa KKKT 1979 - 1992.

Wamisionari walipaswa kupitia Bukoba. Walipofika Bukoba mwaka 1910 wakashawishika kufungua kituo Bukoba na ile nia ya kuanzisha kazi ya mission Rwanda ikawa imesitishwa.

Chama cha tatu kufika nchini Tanzania - Chama cha Misioni cha Leipzig nacho kilitokea Ujerumani kiliingia nchini Tanganyika, kwa wakati huo, mwaka 1893 na kuanza kazi ya misioni Kaskazini ya nchi sehemu ya Kidia, Old Moshi.

Kutokana na vyama hivi vitatu vilivyoanzisha Ulutheri Tanzania, pamoja na mchangano mkubwa wa vyama vingine vya misioni vilivilokuja baadaye kutoka Ulaya na Marekani; Neno la Mungu limeendelea kufundishwa kwa upendo na kwa usahihi.

Shule nyingi za msingi, za kati, sekondari na vyuo vya ufundi na ualimu, zahanati na hospitali vilianzishwa kwa lengo la kumhudumia mwanadamu kikamilifu – kimwili, kiroho na kiakili. Kazi kubwa ya Kanisa la Kilutheri tangu lilipoanzishwa na vyama hivyo nilivovitaja hapo mwanzoni imekuwa ni kufundisha Neno la Mungu na kuhubiri Injili ya Yesu kwa usahihi.



# Injili ilivyoenea Masaini

**Na Mch. Profesa Joseph Parsalaw**

Katika dibaji ya “*Kitabu cha Historia ya Injili Dayosisi ya Kaskazini Kati 1904 hadi 2004*”, marehemu Askofu Dkt. Thomas Laiser alisema: “*Tunapaswa kumshukuru Mungu kwamba, kupitia wamisionari, Mungu amepanda mbegu njema ya Neno lake kwetu.*”

Wamisionari wa Chama cha Leipzig, Ujerumani, waliofika Arusha kutoka Kilimanjaro na Meru walifika kuanzisha stesheni au kituo cha Misioni Ilboru na tarehe 26 Juni 1904 Ibadha ya kwanza eneo la Waarusha ilifanyika.

Wamisionari wa kwanza wa Kilutheri waliotokea eneo la Meru waliingga katika eneo la Waarusha mwaka 1902 wakitokea Nkoaranga, Meru ambapo Mch. Arno Krause, aliyetoka Chama cha Leipzig alikuwa na jukumu la kutafuta eneo la kuweka stesheni ili kueneza Neno la Mungu na huduma za kijamii kwa Waarusha.

Wamisionari wawili Herman Albert Fokken na fundi mjenzi Karl Luckin waliteuliwa na Chama cha Misioni cha Leipzig kuanzisha kituo cha Kanisa eneo la Waarusha. Mch. Fokken aliwasili Kilimanjaro tarehe 23 Julai 1902 akitokea Mombasa, Kenya baada ya kusafiri kwa meli. Alifanya kazi Shira, Machame chini ya Mmisionari Bleicken hadi 1904 alipoitikia wito wa kuanzisha kazi ya Injili Arusha.

Wamisionari Fokken na Luckin walitembea kwa miguu tangu Machame wakiongozana na wabeba mizigo 75 na kufika Meru tarehe 16 Juni 1904. Walipumzika kwa siku nne pale Nkoaranga kabla ya kuanza safari alfajiri kuelekea Arusha ambapo walifika siku hiyo hiyo.

Walipofika Bomani Afisa wake mmoja aitwaye Baron von Reitzenstein aliwapa chakula cha mchana na kuwasindikiza hadi Ilboru. Pale Bomani walipokelewa na kiongozi aliyeitwa Sabaya Orkasis ambaye ndiye alijitolea kutoa eneo la kujenga kituo cha kuanzisha kazi ya Injili ilivoenea eneo la Waarusha, Wamasai, Wairaqw na Sonjo.

Mwaka 1904 Mch. Fokken alimpokea kijana Mwarusha akitokea kituo au stesheni ya Mamba, Kilimanjaro aliyeitwa Sauli Rerei mzaliwa wa eneo la Ilmeshoroori. Kijana huyo akiwa mtoto mchanga alichukuliwa mateka wakati wa vita kati ya Waarusha na Wajerumani walipokuwa wanalipiza kisasi kwa kuuawa mwaka 1896 kwa wamisionari

wenzao yaani Ewald Ovir na Karl Segenbroel kule Akeri, Meru wakati huo eneo hilo likitawaliwa na Mangi Matunda. Rerei alikuwa mtu wa kwanza Mwarusha kubatizwa tarehe 14 Feb 1904 na alipangiwa kufundisha pale Ilboru.

Mmisionari Leonard Blumer alifika Ilboru tarehe 8 Agosti 1907 kusaidia kazi katika eneo lililoonekana kuwa gumi kuingiza Injili. Hivyo Mch. Fokker alisaidiwa na Rerei na Blumer katika kufundisha watoto kwenye vituo vitatu yaani Ilkining'a, Kimandolu na Salei.

Mch. Fokker aliwahi kuelezea namna ilivyoenea vigumu na akaonesha



*Mch. Profesa Joseph Parsalaw  
Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini  
Makumira.*

kukata tamaa kwa jinsi Waarusha walivyosita kupokea Neno la wokovu. Daima aliwasihii marafiki na wote waliokuwa wakitoa misaada yao kwa kazi ya misioni, wasiache kuomba ili Bwana wa Kanisa aimarishe kazi yake. Tarehe 10 Machi 1910 Mch. Fokker alihamia Kituo cha Nkoaranga na kumkabidhi Mch. Blumer kituo cha Ilboru.

Kanisa la Ilboru liliengwa kati ya 1911 na 1915 lilipowekwa wakfu. Na mwaka 1919 neno ‘usharika’ lilianza kutumika rasmi badala ya neno ‘misioni au misheni’. Na wakati huo Ilboru iliwa na washarika 88.

Japo Vita Kuu ya kwanza ya Dunia iliyumbisha kazi ya misioni; wenyeji walichukua kama wajibu wao badala ya kuona kama ni kazi ya wageni peke yao. Maendeleo ya kazi ya Injili tangu 1904 hadi sasa ni tunda la ushirikiano wa dhati kati ya wakristo wenyeji, viongozi wao na washirika au wadau wote toka vyama Vya Misioni na Makanisa dada ya Ulaya na Marekani.

Kufika 1922 kazi ya Injili na elimu zilioneekana kuwa na mafanikio makubwa. Kazi kwa wakati huo iliendeshwa na wakristo wenyeji huku

Mmisionari Mch. Blumer akisaidia hapa na pale maana aliwajibika kwa wakati huo kutunza pia Kituo cha Nkuaranga.

Ujenzi wa kanisa linaloitwa sasa Usharika wa Mjini Kati ulianza mwaka 1914 na kukamilika 2 Machi 1924. Na hapo ndipo kulikuwa na shule iliyojulikana kama Shule ya Bomani.

Hadi mwaka 1927 hapakuwa na madhehebu yo yote yaliyokuwa yameweza kueneza Injili Masaini. Sababu kubwa ni kwamba eneo hilo liliwa na wanyama hatari na kwamba watu waliwaogopa Wamasai kwa ukali wao.

Harambee ya kwanza kwa ajili ya kwenda kuanzisha kazi ya Injili Masaini ilifanyika Ilboru ambapo sh. 475 zilichangwa *Siku ya Mavuno* na washarika. Walichaguliwa Washarika wanen waaminifu na walimu wawili wenye uzoefu na tarehe 3 Julai 1927 waliwekewa mikono tayari kwa safari ya kuelekea Longido, yaani Masai ya Kaskazini na Naberera, yaani Masai Kusini.

Mwaka 1929 Usharika wa Ilboru ulishereheke miaka 25 ya Injili ikiwa na washarika karibu 500. Siku hiyo washarika walijitoa tena kwa kupeleka mapato yao ya siku hiyo ili kupeleka Neno la Mungu Masaini na Injili iliingia rasmi Masaini Kusini 30 Juni 1929.

Kazi ya Injili ilienea hadi Loliondo na Kibaya. Huko Loliondo kituo cha kwanza kilifunguliwa eneo la Arash Septemba 1939. Arash ni umbali wa maili 40 Kusini Mashariki ya Loliondo. Ubatizo wa kwanza Masaini ulifanyika 2 Septemba 1934 ambapo watu wawili walibatizwa. Na baada ya ubaizo huo ndipo Wamasai wa Loliondo wakakubali kazi ya Injili ianze kwao.

Wakristo wa Naberera walishiriki Meza Takatifu kwa mara ya kwanza 4 Aprili 1938.

Misioni ya Masaini ilielekeza nguvu wenye elimu hasa kwa watoto maana kazi ya Injili ilipata vipingamizi vingi ikiwa ni pamoja na utamaduni wa ndoa za mitara kwa watu wa Masaini. Wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia Mch. Lazarus Laiser wajoli wenzake yaani walimu na wainjilisti walichukua mizigo wa kufanya kazi ya Injili Umasaini na Arusha. Tarehe 26 Novemba 1948 kazi ya Injili ilianza Sonjo.

Mwaka 1972 Dayosisi ya Kaskazini iligawanyika na kuunda Sinodi ya Mkoani Arusha ambayo kwa sasa ni Dayosisi ya Kaskazini Kati iliyo katika eneo la Mikoa ya Arusha na Manyara.



# Ujasiriamali kuimarisha ndoa

Baadhi ya familia wanawake walitelekezwa na wenzi wao baada ya maisha kuwa magumu zaidi.

Lakini kuititia mradi huu akina mama hao wameendelea kutunza watoto na kuwapatia elimu kwa kuwalipia ada ya sekondari na vyuo. Wanawake kadhaa toka maeneo mathalani ya Meru, Pare, Lushoto, Ifakara n.k wanatoa ushuhuda

jinsi mradi huu ulivyowarudishia utu na hadhi zao katika jamii kwani walijisikia wanyonge na hawana thamani kabla ya kujunga na mradi.

Baadhi ya wanaume wamerudi na kujunga na familia baada ya miaka zaidi ya kumi ya kutelekeza familia na kukuta akina mama wamejenga nyumba bora na za kisasa.

Ama kweli mradi wa ng'ombe wa maziwa umeleta mageuzi katika jamii kwa kuwajengea uwezo na kuwaleta pamoja wafugaji na wakulima wadogo na watu wasio na tumaini la kupata msaada wa kijamii. Umerejeshea jamii ya watu waliokata tamaa na kukosa msaada hadhi na utu wao.



*Nyumba iliyokuwa inatumiwa na familia ya mkulima huyu ambaye jina lake halikuweza kupatikana na mama yake mzazi (wa kwanza kushoto) kabla hajapokea mtamba. Baada ya kupata mtamba alijiendeza hatimaye akaweza kujenga nyumba yake na mkewe. Pichani kulia ni nyumba nyingine anayomjengea mama yake.*

## Washiriki wanaunda vikundi ili kupata mitaji



*Katibu wa kikundi cha SACCOS, Dayosisi ya Kusini Magharibi, Bw. Daima Ngajilo, akieleza jambo kwa wanakikundi.*

Juu: Aziza Butondo akiwa amembeba ndama wake kwa furaha. Huyu ni mjane (mwislamu) na mnufaika wa mradi katika eneo la Nzega la Dayosisi ya Kati. Chini ni Bw. na Bibi J. Mfinanga waliyopata; walipotembelewa na Mratibu wamejingga na kuanzisha za uzalishaji na katika maamuzi imekuwa mojawapo ya mkazo wakati wa utekelezaji mradi. Tathmini mbalimbali zilizofanyika katika nyakati tofauti zinaonyesha ongezeko la ushiriki wa jinsi zote katika shughuli za uzalishaji na maamuzi ya matumizi ya mapato.



Kutokana na mafunzo wanaume, wanawake, aina ya chakula hata makande bila kutumia gharama kubwa (SACCOS) katika baadhi ikilinganishwa na tulipokuwa ya maeneo. VICOBA na tunatumia jiko la gesi la Orxy SACCOs hizo zimekuwa kwa gharama ya Tshs.40,000/= mkombozi mkubwa kwani kwa kuchemsha chai tu zimewezesha huduma ya kwa kutumia jiko hilo hapo kibenki kupatikana vijiji pembeni." (c) 2012 KKKT/ Patricia Mwaikenda)



# Kupunguza Umaskini

## Jina jipya programu bora zaidi

Malengo ya Programu ya Uhai na Mazingira ni:

- Utunzaji wa mazingira kwa kutoa elimu kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na kuhamasisha jamii kutunza mazingira, kuwezesha uanzishwaji wa vitalu vya miti, upandaji miti na utunzaji. Utunzaji wa vyando vya maji, kilimo kinachozingatia utunzaji wa mazingira na matumizi ya tope chujio(bio-slurry)
- Ugawaji mitamba wa kisasa wa maziwa(heifers) na mbuzi wa maziwa kwa familia zenye kipato duni, wajane/ wagane, yatima, walemvu, wanawake na wasiojiweza kwa ujumla
- Usambazaji wa teknolojia ya nishati ya biogesi kwa kujenga mitambo ili kutunza mazingira kwa kupunguza matumizi ya kuni, mkaa, mafuta ya taa, uchafuzi wa mazingira na uharibifu wa macho (macho mekundu) kwa akina mama kutohana na moshi. Kuwapunguzia wanawake na wasichana adha ya kutafuta kuni na hivyo kuwapatia muda zaidi wa kuendesha shughuli za uzalishaji na masomo
- Kuwawezesha vijana kuijajiri kwa kuwapatia ujuzi wa kujenga mitambo ya biogesi na uanzishwaji na uendeshaji wa kampuni ndogo za ujenzi
- Kuwawezesha familia kupata maji safi na salama ya kunywa kwa kuwapatia kifaa/chombo cha lita 10 kinachochemsha maji kwa kutumia nishati ya jua
- Kutoa elimu kuhusu

utunzaji bora wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa, utunzaji wa mazingira, Jinsia na Maendeleo, Ujasiriamali, Uundaji na uendeshaji wa vikundi (groups formation and dynamics), Uanzishwaji na uendeshaji wa mifuko ya fedha kama VICOBIA, SACCOs nk na masomo mengine kuendana na mahitaji ya jamii katika maeneo ya programu

### MAFANIKIO

Mpaka sasa programu imefanikiwa kutekeleza

mambo yafuatayo:

- Wananchi 43 wamepatiwa mafunzo ya uendeshaji wa programu kwa kuzingatia haki na usawa (implementation of the programme through Rights Based Approach), kamati 11 toka maeneo mbalimbali ya programu zenye wajumbe 143 zimepatiwa mafunzo ya uendeshaji na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za programu
- Wafugaji 130 wamepatiwa elimu ya

utunzaji bora wa ng'ombe wa maziwa, mitamba wa maziwa 130 na madume 13 wamegawanywa kwa familia za wafugaji hao katika maeneo ya Mpanda, Nzega, Kahama, na Manyoni.

- Mitambo ya biogesi 801 imejengwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.
- Vifaa vya kuchemsha maji 60 vimegawanywa kwa familia 60 katika maeneo ya Kahama.

## Mradi wa ng'ombe wafikia kikomo

Mradi wa Ng'ombe wa Maziwa ulibuniwa kwa kuhakikisha uendelevu unapatikana baada ya uhisani kukoma kwa njia ya kupeana ndama jike wanajamii wameendelea kutekeleza mradi kwa kugawa ndama kwa kila aliyepata mtamba. Pia maeneo mengine yameweza kuanzisha mradi katika maeneo mpya kutumia ndama jike wa kugawanywa. Mfano huko Mngeta (Dayosisi ya Kusini) na Ikuwo (Dayosisi ya

Kusini Magharibi) wafugaji wa maeneo hayo kwa kushirikiana na viongozi wa Dayosisi wameanzisha miradi katika maeneo mapya ya Mkangawalo na Kigala kwa kupeleka ndama na kuwagawa kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mradi wa Ng'ombe wa Maziwa ilibidi ufike kikomo kwasababu kimsingi ni mradi hivyo ulipaswa kuwa na ukomo. Kukoma kwa mradi huu kumeliwezesha Kanisa la Kiijinjili la Kilutheri Tanzania

kuanzisha Programu ya Uhai na Mazingira (Sustainable Livelihood and Environmental Programme). Kuanzishwa kwa programu hii kumeendeza baadhi ya shughuli zilizokuwa zinafanyika chini ya Mradi wa Ng'ombe wa Maziwa. Awamu ya kwanza ya Programu hii ilianza kutekelezwa rasmi Julai 2011 na ni ya miaka 2½, mpaka 2013 na kufuatiwa na awamu ya pili ya utekelezaji ya miaka minne kuanzia 2014 – 2017.



Picha juu: Baba Askofu Mameo Ole Paulo, Mkuu wa Dayosisi ya Morogoro, akizungumza na familia ilionufaika na mradi eneo la Lugoba Jimbo la Chalinze. Katika eneo hilo jumla ya familia 87 zimenufaika mpaka hadi Juni 2013.

# Mafanikio na mawazo juu ya kuinua viwango

MIAKA  
50  
KKKT

Tathmini ya Mpango ilifanywa na Dkt. Sydney Ndeki, Bw. Clement Kwayu, Dkt. Aikande Clement na Dkt. Declare Mushi kwa kutembelea hospitali 12 za KKKT; Ofisi Kuu ya KKKT; Dayosisi za KKKT na CSSC. Tathmini ilifanyika tarehe 9 Agosti hadi 2 Septemba 2012:



Washiriki wa mukutano wakijadiliana katika vikundi.

Pamoja na mafanikio yaliyotajwa, kurasa zilizotangulia, na hatua kubwa kupigwa na Kanisa katika sekta ya afya; kuna mapungufu na changamoto zilizojitokeza wakati washiriki walipojadili ripoti.

## Malengo ya Mpango wa Afya Endelevu KKKT

Malengo ya awamu ya tatu yalikuwa:

1. Kujenga uwezo kwa viongozi wa vituo vya afya vya Kanisa (kujua kupanga, kutekeleza na kutathmini) kazi za kuzuia maradhi na kutibu.
2. Kufanya utetezi kuimarisha utekelezaji wa sera ya PPP katika sekta ya afya, ili vituo vya Kanisa viweze kupoke mgao wa msaaada wa fedha toka Serikalini.
3. Kuinua kiwango cha huduma za afya katika vituo vya afya vya KKKT.
4. Uendelevu wa huduma za afya.

## *Maoni ya washiriki ili kuboresha huduma katika vituo vya Kanisa:*

Kanisa limeshauriwa kuhakikisha linatafuta njia mbadala za mapato ya kutosha kuendeleza huduma endapo sera ya taifa ya PPP itafikia mwisho. Njia mojawapo ni kwa vituo vya afya husika kushawishi watu au makundi yajiunge na mifuko ya bima ya afya kama njia moja wapo ya uhakika kwa hospitali kuingiza kipato.

Mkurugenzi wa CSSC alisema wamependekeza Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iware kibali cha kuandaa mwongozo kwa hospitali za rufaa ngazi za mikoa na kwamba KKKT inaalikwa kushiriki.

Shirika la Madawa



Wawezeshaji wa majadiliano kuhusu Ripoti ya Mpango wa Afya Endelevu KKKT. Aliyesimama ni Dkt. Aikande Clement, Bw. Clement Kwayu (katikati) na Dkt. Sydney Ndeki.

(MEMS) linahama toka KKKT na kuhamia CSSC ili kuboresha muundo wake.

### KUINUA KIWANGO CHA HUDUMA NGAZI YA KITUO NA DAYOSISI:

- Waajiriwe watumishi wenye sifa katika ngazi zote: tiba, uuguzi, uhasibu, uagizaji madawa na teknolojia ya habari na mawasiliano.

- Katika ngazi ya dayosisi wataalam wenye ujuzi fani za afya na uongozi ndio wachaguliwe kuwa wajumbe wa bodi za tiba.
- Jambo muhimu ni kutafuta jinsi ya kurahisisha upatikanaji wa huduma ya maji, nishati na usafiri. Ili kufaulu katika hili la watumishi ni vema kuwapa mafunzo watumishi vijana; kuwapa mafunzo mafupi mara kwa mara pia kuwafunza kwa vitendo. Kila dayosisi ipange vivutio kama kutoa posho za ziada, kuwa na mazingira mazuri ya kazi, kuwapa watumishi mikopo na nafasi ya kuijiendeza kitaaluma.



Dkt. Declare Mushi.

### KUBORESHA HUDUMA KATIKA VITUO:

- Ni muhimu kuimarisha huduma za kinga, tiba, upasuaji salama, nk.
- Kufuata miongozo kama matumizi sahihi ya dawa, kutumia miongozo ya upasuaji na kuzuia maambukizi
- Bodii za Afya za vituo ziajiri watumishi wenye sifa na wenye moyo wa huduma
- Pawepo kiasi cha kutosha cha madawa na vifaa tiba
- Hakikisha watumishi wanapata mafunzo kila mara
- Mafunzo kazini yaendelee kutolewa kila wakati na kusaidia usimamizi na ufuatiliaji.

# Mradi wa Tiba Shufaa KKKT

Na Dkt. Zebadia Paul Mmbando

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), limekuwa likitoa huduma mbalimbali kwa jamii ikiwemo huduma ya tiba shufaa (huduma kwa wagonja wenyewe magonja sugu na ya muda mrefu ikiwemo kansa na UKIMWI) kwa miaka zaidi ya 50 ambapo hospitali 20 za KKKT zinatoka huduma hii. Ufadhilli mkubwa wa mradi huu unatolewa na kanisa la Kilutheri Marekani. Mradi huu umefanikiwa kuunganisha hospitali zinazotoka huduma ya tiba shufaa na huduma ya wagonja majumbani na taasisi zinazotoa huduma kama hiyo nchini marekani (*Hospice partners*) ambapo zaidi ya hospitali 16 za KKKT zimeunganishwa na mpango na kupokea misaada mbalimbali kwa mfano: madawa, fedha, magari, nafasi za masomo na fursa kwa watumishi wa hospitali za KKKT, nk. Kufanya ziara Marekani ili kupata uzoefu zaidi kuhusu tiba shufaa mionganoni.



Mmoja wapo wa watumishi wa Mradi wa Huduma ya Tiba Shufaa KKKT, Bibi Anna Mahenge (kushoto) akimnasihii mgonjwa wakati wa mzunguko kwa ajili ya huduma za wagonja majumbani kwao.



Maonyesho yaliyoandalila na Vitengo vya Afya KKKT na washirika wa Kanisa katika sekta ya Afya. Walionesha vitu mbalimbali au mabango ni kama vile Kitengo cha Malaria, Huduma ya Afya ya Msingi, Mradi wa Kufuatalia viwango vya huduma katika vituo vya KKKT, nk.



Ufunguzi wa Hospitali ya Bulongwa ulihudhuriwa na Mkuu wa kwanza wa KKKT, Askofu Dkt. Stefano Moshi na Katibu Mkuu Bw. Joel Maeda.


wagonja kiuchumi ikiwemo kuhimiza wagonja kuijingiza kwenye vikundi nya kuweka na kukopa ili kujiongezea vipato vyao imepewa kipaumbele. Elimu kuhusu Chakula bora, elimu ya kinga na kuzuua maambukizi mapya ya VVU kwa walioathirika imekuwa ikitolewa na mradi huu tokea awali.

Hivi karibuni, wagonja wengi wameripotiwa kukosa ufasi mzuri wa dawa za ARV na wengine wameonekana kupotea kwenye huduma hiyo. Watoa huduma ya tiba shufaa pamoja na huduma kwa wagonja nyumbani wameonekana kuwa msada mkubwa hivyo mradi umekuwa ukihamasisha mahusiano ya kiutendaji katy ya Huduma ya tiba shufaa na Huduma ya wagonja wa nyumbani (HUWANYU) pamoja na Vituo vya tiba na huduma ya VVU ili kusaidia upatikanaji wa wagonja waliopotea katika huduma ya dawa za kupunguza makali ya VVU ili kuwarudisha kwenye huduma.

Kuhusu suala la maumivu kwa wagonja wenyewe magonja sugu kama kansa, ukimwi, nk., tiba shufaa inahusika sana katika suala hilo. Mradi huu umewezesha hospitali 19 za KKKT kuwa na kibali cha kutoa dawa ya 'morphine' kwa Wagonja wenyewe maumivu makali. Dawa hii imekuwa msada mkubwa sana kwa wagonja kwa ajili ya uwezo wake mkubwa wa kutibu maumivu makali na pia bei yake kuwa rahisi.

Ili kuhakikisha uwepo wa huduma hizi kwa muda mrefu, mradi wa Tiba Shufaa wa KKKT umejenga ushirikiano na taasisi mbalimbali ambazo zimekuwa zikiwezesha muendelezo wa huduma hii. Pia mradi umetoea mapendekezo ya kuwepo na kiasi kidogo cha mchango wa kifedha kutoka kwa wagonja au familia za wagonja wanaojimudu kiuchumi kwa hospitali husika, mpango huu utaruhusu umilikishwaji wa huduma kwa jamii husika na pia kuongeza kipato ili kuinua na kuimarisha huduma ya tiba shufaa kwa KKKT na Tanzania kwa ujumla.

## BODI YA KWANZA YA AFYA



Bodi ya Afya KKKT ilikutana kwa mara ya kwanza Hospitalini Haydom 1974. Wanne toka kushoto ni Bw. Joachim Macha aliyekuwa Katibu wa Utabibu, KKKT.



# Kitabu kipyä kinakuja

*Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) katika kuadhimisha kumbukumbu ya miaka 50 itatoa kitabu Kiitwacho: "Umoja na Utambulisho Wetu" ambacho ni kwa ajili ya viongozi ngazi zote kukumbushana kuhusu maandiko ya msingi ya umoja wa KKKT. Ifuatayo ni nukuu kwa ufupi ya baadhi ya mada:*



## Neno pekee, Kristo pekee, Imani pekee na Neema pekee

Mwasisi wa Ulutheri, Dkt. Martin Luther, anatuambia Kristo pekee ndio msingi wa kuwepo Neno pekee. Yaani pasipo Kristo hata fundisho la Neno pekee halina mashiko. Na kwamba Kristo ni ufunuo wa Mungu na pasipo Yeye tusingemjua Mungu kwa jinsi tunavyomwona kwa njia ya Kristo.

Kanisa kama taifa la watu wa Mungu waliomkubali Yesu Kristo kuwa Bwana na mwokozi wao na kuingia katika taifa

hilo kwa njia ya ubatizo, hufanya hivyo kwa kufuata Neno la Mungu.

Kuhesabiwa haki hakutokani kwa namna yoyote na jinsi mtu anavyowezza kumpendeza Mungu ama kwa ajili ya utakatifu wetu au kwa matendo yetu mazuri. Bali kuhesabiwa haki kwetu ni kipawa cha Mungu mwenyewe. Tumesamehewa na kuhesabiwa haki katika Kristo. - **Askofu Dkt. Steven Munga**

## Ukuhani wa waaminio wote

Wapo watu wanaodhani kuna watu walio na mawasili ya moja kwa moja na Mungu kuliko wengine kiasi kwamba wako radhi hata kutoa fedha ili waombewe na hao "mitume-viunganishi". Kwa upande mwingine kuna wanaofikiri kwa kuwa ukuhani ni kwa waaminio wote; basi wao hawahitaji tena kuwa na wachungaji au daraja la uchungaji.

Fundisho la ukuhani wa waaminio wote hupinga mafundisho yasiyo ya Kiblia yanayositisiza Wachungaji au makasisi wanao upekee wa kitabaka

## Utaratibu wa Ibada

Taratibu za ibada ni moja ya utambulisho wa dhehebu au dini husika. Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani ambayo kwa sasa lina wanachama karibu milioni 70.5 lina taratibu za ibada ambazo kimsingi zinapanana. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri hali kadhalika likizingatia mambo ya msingi yanayofanana katika Ibada zetu zitatutambulisha kwamba sisi sote ni wakristo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Umuhimu wa kuwa na utulivu na unyenyekevu kimwili na kiroho ibadani ni mambo yanayoonesha umoja na heshima kwa nyumba ya ibada. Na haya yanatarajiwa toka kwa washiriki wote kuanzia viongozi wa Ibada wenywewe, wana kwaya, wazee na washarika. Yakuzingatia ni kuanzia uvajji, usumbufu au kuingiza mambo ya kuiga iga toka sehemu au madhehebu mengine kama mtindo wa maombi, nk. - **Askofu Elisa Buberwa**

kwa mambo ya kiroho na kiwango cha utakatifu. Dkt. Martin Luther alipokongomea Hoja 95 katika Kanisa la Kuu la Wittenberg tarehe 31 Oktoba 1517 pamoja na mambo mengine, aliyakataa mafundisho hayo aliposema: kila mkristo anayejutia na kutubu kweli dhambi zake anayo haki ya kusamehewa dhambi hata pasipo hati.

Ungamo la Augsburg linaweka wazi kwamba Wachungaji au makasisi ni wakristo kama wenzao ila wametengwa kwa kuwekewa mikono ili kuongoza Usharika, kusimamia, kufundisha Neno la Mungu na kutoa sakramenti.

Pia Mkristo wa kawaida hayuko chini ya kongwa la ye yote yule anayejiwaka kuwa kiunganishi kati yake na Mungu. - **Mchg. Dkt. Frederick Shoo**

## Utoaji wa Kikristo

Matoleo ni sehemu ya ibada ya Kikristo. Katika Agano la Kale waabuduo walikwenda mbele za Mungu wakati wa Ibada na matoleo yao. Na Mungu aliwakirimia wema kwa kuwapa raslimali ambazo walizitoa kama sadaka kumshukuru Mungu. Utoaji wao ultoka na utambuzi wa nguvu ya Mungu. Hawakutoa kwa namna ya "kupanda mbegu ili uvune matunda." Walitambua jinsi Mungu alivyowakirimia mali na kuwapa ulinzi. Kwa unyenyekevu, hiari na kwa moyo walitoa mali zao nzuri na kwa wingi. Hawakutoa ili wabarikiwe. Walitoa kwa sababu Mungu alikwisha wabariki tayari, na Mungu aliendelea kuzidisha baraka zake kwao siku hata siku hili ni moja ya tunda la utoaji wa Kikristo. - **Mchg. Ambele Mwaipopo**

## Kuomba katika Jina la Yesu

Tukiruhusu nafsi zetu kuridhika na utendaji wa Mungu katika maisha yetu, ni bora zaidi kwa sababu ile iliyopo Yak. 4:2: "Mwatamani, wala hamna kitu; mwaua na kuona vivu, wala hamuwezi kupata. Mwafanya vita na kupigana, wala hamna kitu kwa kuwa hamuombi! Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu."

Ndivyo ubinadamu wetu ulivyo dhaifu kuhusu maombi. Tena ni heri kujifunza ukweli wa maombi yalivyo kwa sababu maombi yasiyojibwa na Mungu kama tunavyotaka, yaani kama jibu la Mungu kwa maombi yetu ni hapana, tuje na kuamini kuwa hili ni jibu kamili, tena jibu chanya tu.

Tujifunze kuomba vizuri na kwa hakika toka namna na unyenyekevu wa Bwana wetu Yesu Kristo, alivyoomba na kuhitimisha maombi yake kwa maneno "Mapenzi yako yatimizwe." Mt. 26:42: "Baba yangu, ikiwa haiwezekani kikombe hiki kiniepuke nisipokunyuwa, mapenzi yako yatimizwe." - **Mchg. Gabriel Kimirei**

## Mlutheri ni nani?

Martin Luther anasema Kanisa, ni pale ambapo Injili inahubiriwa na kupokelewa na tena Sakramenti ya Ubatizo na Ushirika wa Meza ya Bwana vinatolewa kwa usahihi wake. Mlutheri anamwamini Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yake na kubatizwa katika Utatu Mtakatifu, ambapo anasafishwa dhambi zake na kupokelewa katika kundi la waaminio na kufanyika mwana wa Mungu. Mlutheri anaamini juu ya mafundisho, mafunuo, mapenzi na ahadi za Mungu kupitia Maandiko Matakatifu yaani Biblia, kuwa ndiyo msingi wa maisha yake. Mlutheri anakubali na kuamini ya kuwa Katekismo Ndogo ya Dkt. Martin Luther, ukiri wa Nikea, Mitume, Athanasio na Ungamo la Augsburg lisilobadilika ndio maelezo sahihi tena ya wazi ya Neno la Mungu.

Siku ya kuabudu kwa Mlutheri ni Jumapili; siku Bwana wa Kanisa, Yesu Kristo, alifufuka akiashiria ushindi na ukoo alionao juu ya nguvu ya dhambi na ya mauti (Mathayo. 28:1; Marko 16:2 na Yohana 20:1). - **Mchg. Dkt. Angel Olotu**

# Injili ilivyoenea Ukanda wa Kusini

○ Chama cha Misioni cha Berlin I Kilianzisha kazi ya kueneza Injili Ukanda wa Kusini mwa Tanganyika


Na Askofu Dkt. Owdenburg Mdegella

Kazi ya kueneza Injili Ukanda wa Kusini mwa Tanganyika ina historia inayorudi nyuma hadi mwaka 1899 ambapo Mmisionari wa Kijerumani Mch. Wilhelm Neuberg alianzisha stesheni mahali paitwapo Itonya katika milima ya Udzungwa. Mchungaji huyu aliitwa na wenyeji wa eneo la Itonya kama "Mwambetani" kwa lugha ya Kichehe ikimaanisha mnavuna nini? Hii ilitokea kwa sababu kila alipohubiri alikuwa akiuliza mnavuna nini kutoka kwenye Neno ninalo hubiri. Kazi hii ya Injili iliyoanzishwa na Mch. Neuberg iliwezesha kutokea kwa Sinodi ya Ubena-Uhehe mwaka 1902 ambayo baadaye iliitwa Sinodi ya Kusini.

Chanzo halisi kilichosababisha Injili kuingia Itonya ni kwamba kulikuwa na mtu aliyeitwa Mwamagelanga mzaliwa wa maeneo ya Idete alikuwa anafanya kazi katika mashamba ya chai, Lupembe huko Njombe. Mtu huyu aliamua kumuomba mmisionari mmoja kwa kumwambia kuwa watu wa maeneo ya Itonya wanahitaji Injili, ndipo mmisionari huyo aliyeitwa Neuberg akawaambia wenzake na akakubali kupeleka Neno la Mungu katika maeneo ya Itonya. Inasadikiwa kuwa Wakristo wa kwanza kubatizwa walikuwa Aron Kikoti, Lupituko Mkemwa, Yehoswa Kikoti na ndio waliokuwa walimu na wahubiri wakiwa wanapata posho ya shilingi tano kwa mwezi.

Stesheni nyingine ilianzishwa na Mch. Julius Oelke mahali paitwapo Ilutila katika milima ya Udzungwa pia. Stesheni hii ilipewa jina la Kijerumani liitwalo Neustettin, lenye maana ya 'stesheni mpya', hilo ni jina la mji mkuu wa eneo la Pommern, katika nchi ya Poland ya sasa.

Kufika mwaka 1930 mmisionari mwagine wa Kijerumani aitwaye Mch. Herman Neuberg mtoto wa Mch. Wilhelm Neuberg mwanzilishi wa stesheni ya Itonya alipewa wajibu wa kusimamia eneo la Kikanisa la Ubena-Uhehe na Ulanga makao yake yakiwa pale Pommern katika nchi ya Wahehe



Askofu Dkt. Owdenburg Mdegella,  
Dayosizi ya Iringa

mahali ambapo pia Herman Neuberg alizikwa baada ya kufariki mwaka 1969.

Mch. Martin Nordfeldt kutoka Sweden, akisaidiana na Mch. Herbert Uhlin, alifika Ilula mwaka 1938. Nordfeldt na Uhlin walikuwa wametumwa na chama cha wamisionari cha SEM (Swedish Evangelical Mission). Kwenye utumishi wake Mch. Nordfeldt alishirikiana na mtumishi mwenyeji, Mch. Yohana Nyagawa aliyekuwa Mkuu wa kanisa la Ubena –Uhehe mwaka 1940 mpaka 1941. Juhudi za watumishi hawa ziliwezesha kuanza kwa ujenzi wa nyumba ya ibada katika stesheni ya Ilula pamoja na ujenzi wa shule ya Ilula iliyosimamiwa na Mwl. Tulawona Luka. Baada ya hapo shule zaidi zilianzishwa na walikuwepo walimu wa Kiafrika waliosaidiana na wageni kuanzisha shule mbalimbali.

Kazi ya injili iliyoanzishwa na wamisionari mionganoni mwa Wahehe na Wabena iliwezesha kuanzishwa pia kwa zahanati na shule ya Biblia. Kwa mfano, mwaka 1953 zahanati ya Kilutheri ya Pommern ilianzishwa na mtaalamu wa matibabu aitwae Luhangano Badi; na tarehe 3/2/1953 Shule ya Biblia ya Kidugala ilianzishwa. Shule hii ilipokea wanafunzi wanane wa kihehe waliokuwa wamepelekwa hapo kwa masomo ya uinjilisti.

Kufika mwaka 1957 eneo la Wahehe lilishakuwa na sharika tano za kilutheri ambazo ni Ihemi, Ilula, Idete na Iringa Mjini. Mwaka 1959 uliweka historia ya kipekee kwa sababu ni mwaka ambao

Kanisa la Kiinjili katika Tanganyika ya Kusini lilianzishwa, Kanisa ambalo Rais wake alikuwa Mch. John Nilsson.

Kwa juhudi za Kanisa la Kilutheri zilianzishwa Shule ya Msingi Pommern (1961 chini ya uongozi wa Mwl. Philemon Chambile), na Bomalong'ombe (1963 chini ya uongozi wa Mwl. Abel Chongola). Mwaka 1963 mmisionari Henrik Smedjebacka alichaguliwa kuwa Rais wa Kanisa la Kinjili Tanganyika Sinodi ya Kusini, na mwaka 1964 Zahanati ya Kilutheri Idete ilianzishwa. Mwaka uliofuata 1965 Mch. Lupumuko Lugala aliteuliwa kuongoza jumbo la Iringa-Uhehe na mwaka 1966 Mch. Herman Neusberg alizindua rasmi jengo la ibada lilokolo Iringa mijini.

Mwaka 1967 Mmisionari Ulla Svenson alifungua rasmi shule ya ufundi ya Kilutheri Mafinga na mwaka huo huo Mch. Lunogelo Vuhahula alichaguliwa kuwa Mkuu wa Jimbo la Iringa – Uhehe. Wakati huo eneo la Uhehe lilikuwa na jumla ya sharika saba, zikiwemo sharika za Ismani na Masisiwe. Mwaka 1969 Mch. Herman Neuberg alifariki dunia na kuzikwa Pommern na mwaka 1970 Mch. Allan Chambile alikabidhiwa wajibu wa kuongoza jumbo la Iringa – Uhehe. Jimbo la Iringa lilianza rasmi mwaka 1977 na Mch. Israel Kiponda alichaguliwa kuliongoza. Kwenye mkutano uliofanyika Lupembe mwaka 1979 palifanywa uamuzi wa kufuata uongozi wa kiaskofu katika KKKT Sinodi ya Kusini. Kwenye mkutano uliofanyika Makambako mwaka 1981 Mch. Dk. Yuda Kiwovele alichaguliwa kuwa Askofu wa kwanza wa iliyoukuwa Sinodi ya Kusini na Mch. Levi Nsemwa alichaguliwa kuwa Msaidizi wa Askofu. Viongozi wengine waliochaguliwa ni Ndg. Obadia Kasumba (Katibu Mkuu) wa Sinodi ya Kusini, Henrick Hult (Mtunza hazina) wa Sinodi na Mch. Nicholas Mwachusi kuwa (Mkuu wa jumbo la Iringa).

## Umoja na utambulisho wetu

Kitabu kipyaa ambacho ni nyenzo muhimu kwa wachungaji na wainjilisti kimetolewa na kanisa hivi karibuni. Jipatie Nakala.


# Maombi ya kuanzisha makanisa nje

Baadhi ya makanisa nchi jirani yalianzishwa kutokana na mwaliiko wa wana KKKT amba walipenda wapate huduma za Kanisa lao wakiwa nje ya mipaka ya Tanzania. Kanisa liliitikia wito na hatimaye makanisa kuzaliwa kwa kutuma wamisionari toka Tanzania kwa ushirikiano na makanisa dada na Vyama vya Misioni.

Pia baadhi ya makanisa kama vile Rwanda, Msumbiji na Burundi yalitokana na kurudi kwa wakimbizi ambao walikuwa wakiishi Tanzania kutokana na vita nchini mwao.

Miongoni mwa wakimbizi hao walikuwepo Wachungaji na Wainjilisti amba walijumuika kuunda Kanisa.

KKKT na washirika wenzake yaani makanisa dada na vyama vya misioni wanaendelea kutunza maeneo ya misioni kwa kuunda bodi za misioni, kutuma wamisionari na kutoa misaada ya mafunzo na mahitaji mengine. Kwa mfano KKKT kuna *Sadaka ya Misioni Nchi Jirani*.



Mkuu wa Kanisa la Kilutheri Uganda Mch. Elisa Bagenyi (kushoto alipoongoza ujumbe wa watu watatu kutembelea KKKT hivi karibuni).

## WASHIRIKA

MIAKA  
50  
KKKT

# Uhusiano wa KKKT na Fungamano

### *Na Mch. Dkt. Elieshi Mungure*

Uhusiano kati ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) umekuwepo kabla ya mwaka 1963. Makanisa ya Kilutheri ya (Tanganyika) yalikuwa wanachama wa fungamano kabla KKKT kuundwa.

Taarifa za Mkutano Mkuu wa Makanisa ya Kilutheri ya Afrika uliofanyika Marangu 1955, zinasema kuwa Kanisa la Kilutheri Tanganyika ya Kaskazini walikuwa wanachama wa fungamano.

Tunamshukuru Mungu kuwa baada ya kuundwa kwa KKKT, mwaka mmoja baadaye walijunga na FMKD na tokea wakati huo wamekuwa wanachama waaminifu wakishirikiana na makanisa mengine ya Kilutheri duniani kueneza Injili ya Yesu Kristo pamoja na kuhudumia mwanadamu kiroho, mwili na kiakili. Uhusiano huu umeendelea kujengeka na kukua sana kwa jinsi ambavyo KKKT imechangia sana misioni na huduma za kidiakonia na maendeleo ya *Kazi za Pamoja* katika fungamano kwa njia na vipawa mbalimbali.

Mfano KKKT imetoa

mchango mkubwa wa watumishi wake kutumika katika nafasi mbalimbali za fungamano kama Marehemu Askofu Dkt. Josiah Kibira, aliyekuwa Rais wa fungamano kwa kipindi kirefu hadi 1984. Ni katika wakati wake pia mambo mengi makubwa yalisifiwa katika fungamano, mfano uamuzi wa kuwa na uwakilishi sawa kwa wanawake, wanaume na vijana katika vikao vya maamuzi vya Kanisa.

Wengine waliotumika katika nafasi mbalimbali katika FMKD ni pamoja na Askofu Amon Mwakisunga, Dkt. Anza Amen Lema, Bw. Elias Sawe, Askofu Dkt. Hance O. Mwakabana, Mch. Anna Makyao, Bibi Doris Kitutu, Askofu Dkt. Alex Malasusa, Mch. Dkt. Elieshi Mungure na wengine wengi.

Fungamano la Makanisa ya Kilutheri duniani pia linashirikiana na KKKT katika kuelimisha watumishi wa Kanisa katika fani mbalimbali ikiwemo theologia, afya na diakonia, uongozi na miradi na maendeleo. Pia miradi ya jamii na maendeleo imekuwa sehemu ya msingi sana ambako KKKT

wameshirikiana kwa pamoja katika kutoa huduma kwa jamii. Pia FMKD linatambua mchango wa KKKT katika kuanzisha na kulea makanisa mengi ya Kilutheri katika bara letu. Huu ni ushuhuda pekee kuwa nuru ya Injili ya Yesu Kristo imewafikia wengi kuititia milango mbalimbali ya KKKT.

Wakati huu KKKT inapo sherehekeea miaka 50 ya kazi ya Injili kwa pamoja, Fungamano la Makanisa linaungana nao wakikumbuka kuwa ni wakati huu pia sisi sote pamoja na makanisa mengine tunakumbuka safari kubwa ya *Matengenezo ya Kanisa* (reformation celebration).

Katika mwaka 2015, makanisa ya Kilutheri Afrika yameamua kwa pamoja kusherehekeea siku hii ya miaka 500 ya *Matengenezo ya Kanisa* kwa kukumbuka miaka 60 tangu Mkutano Mkuu wa kihistoria uliokutanisha Walutheri wote wa Afrika kule Marangu.

Hili linaonyesha ushuhuda na mchango mkubwa wa KKKT katika maisha ya Fungamano na kuwa kiungo muhimu kwa kazi ya Injili duniani.

## Washirika wa KKKT

Kazi ya Injili kueneza Ulutheri haikufanywa na KKKT peke yake bali ilipokea kazi kubwa iliyokuwa ikifanywa na vyama vya misioni toka Ulaya na Marekani. Baada ya KKKT kuundwa iliendelea kutekeleza *Utume wa Mungu* kwa misaada toka washirika wa kazi hii yaani makanisa mama na vyama vya misioni na bado uhusiano unaendelea:

Makanisa mama ni pamoja na:

1. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Bavaria
2. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Northelbian
3. Kanisa la Kilutheri Misioni la Berlin
4. Kanisa la Kilutheri Sweden
5. Kanisa la Kilutheri Finland
6. Kanisa la Kilutheri Norway
7. Kanisa la Kilutheri Denmark
8. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani

Vyama vya Misioni vinavyoshirikiana na KKKT ni kutoka Denmark, Finland, Ujeruman, Sweden na Marekani.



# Misioni kwa Pamoja

Sio siri kwamba wakati Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) linaunganisha makanisa saba kuwa kanisa moja kila kanisa lilikuwa na tofauti za hapa na pale kutokana na makanisa mama yaliyoingiza Injili kati ya mwaka 1987 na 1911. Lakini ulipofika mwaka 1963 viongozi waliamua kuweka tofauti kando na kuunda Katiba moja. Zifutazo ni habari picha kuonesha baadhi ya mambo yanayoimarisha umoja huo.



Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Malasusa akiwa katika picha ya kumbukumbu ya maaskofu watatu waliowekwa wakfu mwaka 2013. Kulia ni Askofu Lucas Mbedule aliyewekwa wakfu kuwa Askofu wa Dayosisi mpya ya KKKT Dayosisi ya Kusini Mashariki Mei 2013; akifutiwa na Askofu Emmanuel Makala aliyewekwa wakfu Mei

2013 kuongoza Dayosisi mpya ya Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria na Askofu Dkt. Alex Mkumbo aliyewekwa wakfu Januari 2013 kuongoza KKKT Dayosisi ya Kati.

Mara baada ya KKKT kuunda Kanisa moja, viongozi walikubaliana makanisa yawe Sinodi au Dayosisi za Kanisa. Vigezo vya Sinodi/Dayosisi kugawanyika ili kuunda

## Ushirikiano

Viongozi wa KKKT wamejipangia wajibu katika masuala ya uongozi kiasi kwamba maaskofu wote huwepo wakati wa matukio makubwa ya kikanisa. Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa (kulia), akisoma hati kabla ya kumkaribisha Mkuu wa KKKT kuzindua Dayosisi Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria.



## Kazi zinaungwa mkono na Serikali

Kanisa limekuwa na sauti na nguvu katika kutelezea mambo pamoja miongoji mwa mapatano ya uthubutu ni kwa kanisa kuwa taasisi ya kwanza binafsi kuanzisha mchakato wa kuwa Chuo Kikuu. Katiba ya nchi imeweka bayana uhuru wa kuabudu kwa hiyo Kanisa kwa kiasi kikubwa imefanya kazi zake kwa ufanisi. Serikali inatambua mchango wa kanisa katika kulea watu wake kiroho na kwa huduma kama afya na elimu. Yote yamewezekana kwa msaada wa Mungu na kutokana na ushirikiano na vyombo vya dola na viongozi wake. Kanisa halikusita kushiriki katika maamuzi na sera za Serikali kwa manufaa ya jamii na halikusita kukutana na uongozi wa serikali kwa masuala ya mustakabali wa taifa. Rais wa Tanzania Dkt. Jakaya Kikwete na viongozi wengine kama Makamu wa Rais Dkt. Mohamed Gharib Billal (kushoto), Waziri Mkuu, mawaziri na viongozi ngazi zote wanashiriki katika kazi na sherehe za KKKT.



**Makamu wa Rais Dkt. Mohamed Gharib Billal akitoa hotuba siku ya kuzinduliwa KKKT Dayosisi Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria.**

mpya viliwekwa katika Katiba. Dayosisi za KKKT ni 22 kwa sasa.

Vyama vya Misioni na Makanisa rafiki yaliunda Vyombo vya Pamoja kutekeleza Utume wa Mungu wa kuendeza Injili ulimwenguni. LCS na baadaye LMC ni vyombo vilivoundwa kuratibu, kupanga, kuweka taratibu za utekelezaji na ufuutiliaji wa masuala kuhusu masomo, miradi ya maendeleo ya jamii, upatikanaji, matumizi na uwakili wa fedha na rasilimali.

Vikao vya pamoja vya washirika wa KKKT havikusau utume mpana zaidi kwani majadiliano yalihusu nchi jirani. Hivyo KKKT imewaunganisha washirika wake ili kufanya kazi pamoja ya misioni nchi jirani.

## Uinjilisti kwa redio

KKKT imejiwekea sadaka maalum kwa ajili ya misioni nchi jirani. Kanisa la Kongo ni ushuhuda wa jinsi kwa njia mbaimbali hata kwa njia ya redio. Viongozi wa Kanisa la Kongo waliposikia Redio Sauti ya Injili (RSI), mjini Moshi iliyokuwa ikipatikana kwa masafa mafupi (SW) walivutiwa na mafundisho yaliyotolewa.

Walisafiri kupitia Rwanda wakaambiwa waende Nairobi ambako nao waliwaelekezwa waende Dar es Salaam na hatimaye wakaelekezwa wafike Moshi maana walikuwa wakitafuta redio iliko ili wajiunge na Kanisa husika. Baada ya kuanzisha uhusiano huo ndipo hatimaye pakawa na Kanisa la Kilutheri Kongo. Redio sauti ya Injili ilianza 1964.

## Huduma ya Injili kwa wakimbizi

Miaka ya 1970 hadi 2000 Tanzania ilipokea wakimbizi wengi sana toka nchi zilizokuwa vitani kwa kuwa nchi yetu ilikuwa kisiwa cha amani. Wakimbizi walitoka Burundi, Rwanda, Msambiji, Zimbabwe, Afrika Kusini, nk. Mwaka 1995 Tanzania ilikuwa na zaidi ya wakimbizi 400,000.

Shirika la Kuhudumia Wakimbizi kwa wakati huo yaani (TCRS) liliandika barua kuomba kama KKKT itoe huduma za kichungaji katika makambi hayo. Na ukawa mwanzo wa mbegu ya Injili kwa nchi jirani.

**MIAKA  
50  
KKKT**

## NGUVU YA KUSAMEHE NA KUSAHAU

# Kusamehe, kuachilia, kusahau - mafundisho ya Yesu: “Samehe saba mara sabini,” *Mathayo 6:9ff*

Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao na Baba yenu wa mbinguni atawasamahe ninyi.

Watu wengi katika Kanisa la leo wana tatizo ndani yao: Tatizo la kutosamehe. Wanatali, wanatoa sadaka, n.k., ati mpaka tupatane mbinguni.

Neno hili lina nguvu kwa sababu Mungu aliutoa uhai kwa makosa yetu, nasi tumesamehewa. Tatizo tulilonalo sisi tuliosamehewa kwa thamani ya kifo (*damu na uhai*) *wa mwana wa Mungu*, ni kutosamehe.

Una kipaji cha uimbaji au lolote lile – bila kusamehe sahau mbingu. Watu ambaa hawajasameheana hawaingii mbinguni. Unajua watoto wanapatana hata kama wazazi wao wa pande mbili wana ugomvi. Sisi tunawakoroga na kuwaingiza kwenye ugomvi wetu. Bila kusahau hakuna amani. Wengi hawawezi kukaa pamoja, kisa wana ugomvi. Wengine wanana kwa lugha na kwa ufundi sana katika maombi lakini hawajasameheana na wenzaa.

Hivi ni nani anakudanganya kuwa hayo ni tiketi ya mbinguni?

Yesu alichuruzika damu na kutoa uhai lakini akasema: “*Usiwahesabie dhambi hii.*” Stefano hali kadhalika alisema: “*hawajui walitendalo uwasamehe.*” Tusiwe na ulokole wa unafiki. Mlokole mnafiki asili yake: Balokole yaani ‘*watu wasio na mbele wala nyuma.*’ Watumishi wanawaombea watu wanapita lakini waombaji hawapiti. Hawasalimiani, hivyo hawapiti wakati mwingine wanajiosha mbele za watu lakini ndani ni tatizo kubwa sana. Watu kusameheana na kuachiliana ni lazima.

Hakuna mahusiano ya mtu na Mungu bila msamaha: Marko 11:25, “*Nanyi kila msimamapo kusali sameheni.*” Kinyume cha hapo Mungu hatasamehe. Ukisimama po pote kusali hakikisha huna mtu uliyemfunga moyoni mwako.

Wengine wanasmama kanisani, kwenye jumuiya au nyumbani kusali lakini sala hiyo haiendi kwa Mungu kwa sababu ndani yake amebeba chuki badala ya Yesu. Hivyo hawaoni neema ya Mungu mpaka hapo atakapo achilia

watu aliowafunga ndani yake. Nguvu mbaya ndani ya moyo ya kifungo cha chuki inasimamiwa na shetani.

Baba, Mwana na Roho Mtakatifu hawata kusamehe wewe usiposamehe wale unaokaa na kuhusiana nao. Sharti wasamehe kwanza ndipo wewe usamehewe. Yoh 9:3 tunasoma: “**Mungu hawasikii wenyе dhambi.**” Chuki ni sehemu ya dhambi. Unapotembea na watu moyoni na huwaachilii ni dhambi. Heri ufanye haraka kabla Yesu hajawahukumu. Unapomshusha mtu au kumtukana mtu kwa siri ni dhambi.

Watu wanaweka ukuta kwa ajili ya wenzaa. **Huwezi kuondoa kibanzi ndani ya jicho la mtu wakati wewe una boriti. Toa boriti lako kwanza halafu kibanzi chake.** Huwezi kumpenda Mungu wakati hujampendeza unaemwona. Huwezi kumpenda Mungu na jirani yako humpendi. Kumchukia mtu ni kujibebea dhambi.

Nguvu ya kusamehe na kuachilia

Kusamehe ni lango, na kutosamehe ni lango. Musa alikuwa na wana wa Israel walikuwa wanamwona Mungu wazi wazi. Kwenye matendo makuu baharini.

Walipokengeuka na kutengeneza ndama, Mungu akachukizwa kwa kukosewa. Lakini Musa akasogea mbele za Mungu kuomba msamaha. Na Mungu alisamehe. Hakuona namna ya kuendelea kutosamehe. Yesu Kristo

alipoteswa alisamehe yote. Hakuna jinsi. Kusamehe, kuachilia na kusahau ni lango la kuingilia katika ndoa, biashara au hali ngumu ya maisha yako. Mtu ambaye hayuko tayari kusamehe, kuachilia na kusahau ni lango la mapepo.

Ukiwa umechukia mtu mapepo yanaingia kirahisi. Mume umemweka moyoni, mfanyakazi na wengine wengi. Mungu akishuka anaona moyo wako ni jalala, mahali pa kutupia uchafu, (maganda ya ndizi, mabaki ya chakula, matakataka). Hapo ndipo Mungu anakosa mahali pa kuingia. Linda moyo wako usiwaweke watu wanaokwaza.

Kutosamehe ni lango la magonjwa kuingia (pressure, kisukari, n.k) Utakufa kabisa usipo wasamehe, achilia na kusahau. Utawaweka wangapi moyoni? Raha jipe mwenyewe. Adui na watesi wako wasamehe bure. Adui zangu niwasamehe bure. Miyo yetu inatakiwa iwe na amani, isiwe na mashaka, iwe na furaha.

Utawaweka wangapi katika moyo? Matukio ni mengi duniani. Wanaotuudhi ni wengi sana. Mkaribishe Yesu kwa usalama wa moyo wako. Wanaokasirika na kufanikiwa kwako ni wengi sana. Miyo inawakera. Hao ni wengi kuliko watu wema. Utawaweka wapi? Jifunze kufungua milango ya kusamehe kuachilia na kusahau.

*Mwandishi Mchg. Rachel Axwesso, ni Naibu Katibu Mkuu Huduma za Jamii, KKKT na ni mwandishi wa vitabu. Wasiliana naye kwa barua pepe: rahelijo@yahoo.com*



*Kwaya mojawapo wakati wa uzinduzi wa Tawi la Mbeya la Chuo Kikuu cha Tumaini. (c) 2013 KKKT.*

# Kanisa linatambua umuhimu wa elimu

## ● Mavuno ni mengi ...watendakazi ni wachache

Katika makala haya yaliyoandikwa na Mchg. Abdiel Ndosi tunapenda kuwapa mfano wa vituo vichache vyta elimu vilivyoanzishwa na Kanisa nchini.

Lutheran Junior Seminary Morogoro (LSJ) ni kituo cha elimu chini ya Kazi za Umoja za Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) chenye madhumuni ya kuelimisha wakristo wa marika yote kwa utumishi katika kanisa na umma kwa kuweka msingi wa Kikristo katika maisha yao ili wamshuhudie Kristo kwa mwenendo wao.

Kuanzia miaka ya 60 uongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ulianza kutoa mafunzo kwa watendakazi wake ili waweze kuchukua nafasi za uongozi katika Kanisa. Hatua

kwa hatua Idara mbalimbali na hatimaye kazi za uongozi wa Sharika na Dayosisi na Ofisi Kuu ya KKKT zikaanza kuongozwa na wana KKKT.

Mahali ambapo kituo cha Kanisa kilipoanzishwa kulikuwa na utambulisho wa vitu vitatu vikubwa: jengo la Kanisa, pili shule na tatu kituo cha tiba au zahanati. Madhumuni ya shule zilizofunguliwa na kanisa yalikuwa mawili - kwa ajili ya watoto wa wamisionari na kwa ajili ya kupata watendakazi kwa nafasi mbalimbali. Baada ya kuwepo shule za kanisa, uongozi ukatambua haja ya kuanzishwa kwa vyuo vyta ualimu pia.

Hitaji la mafunzo ya aina mbalimbali lilifanya viongozi waone umuhimu wa kuanzisha vyuo mbalimbali kwa

Kauli mbiu ni: *Kumcha Bwana ni Chanzo cha Maarifa*, (Mith 1:7).

Tarehe 5 Januari 1969 Lutheran Junior Seminary ilianza huko Kinampanda Singida. Mwaka 1973 ilihamia Vuga, Lushoto. Novemba 1975 shule ilihamia Morogoro mahali ilipo sasa. Eneo la seminari ni eka 125(74ha). Shule iliendelea kukua na kwa sasa shule ina vitengo vifuatavyo: Sekondari(1969), Uongozi (1979), Kilimo 1979), Lugha na Maelekezo (1980), Chekechea (1980).

Tangu kuanzishwa kwake seminari imekuwa chini ya viongozi wafuatao: Bw. Samson Msemembo, Askofu Dkt. Sebastian Kolowa, Askofu Stephano Msangi, Askofu Dkt. Hance Mwakabana, Mchg. Cyprian Yakobo, Mchg. Herb Hafermann, Mwl. Raphael Mwambashi, Mchg. Owens Mwasamwaja, Bw. Estomih Merisali, Mwl Asheri Malekela (Kaimu), Mchg. Dkt. George Fihavango, Mchg. Laison Saning'o (Kaimu) na kwa



Lutheran Junior Seminary Morogoro (LJS).

### Shule 10 bora KKKT zapata vyeti

Halmashauri Kuu ya KKKT imetunuku vyeti kwa shule 10 bora za Kanisa kama ifuatavyo kutokana matokeo ya Kidato cha Nne 2012:

1. Seminari Ndogo ya Kilutheri Agape (Dayosisi ya Kaskazini)
2. Seminari Ndogo ya Kilutheri Ailanga (Dayosisi ya Meru)
3. Kidugala Sekondari (Dayosisi ya Kusini)
4. Seminari Ndogo ya Kilutheri Morogoro (Kazi za Umoja KKKT)
5. Karagwe Sekondari (Dayosisi ya Karagwe)
6. Ugumbilo Sekondari (Dayosisi ya Kusini)
7. Peace House Secondari (Dayosisi ya Kaskazini Kat)
8. Sekondari ya Kilutheri Bukoba (Dayosisi ya Kaskazini Magharibi)
9. Bangala Sekondari (Dayosisi ya Kaskazini Mashariki)
10. Moringe Sekondari (Dayosisi ya Kaskazini Kat)

mafunzo ya theolojia, stadi za ufundi, kilimo, nk. Kutokana na hospitali, vituo vyta afya na zahanati zilipoanzishwa pakawa na haja ya kuwa na mafunzo ili kupata waganga, wauguzi na wakunga, nk.

Tukigeukia LJS, malengo ya LJS ni pamoja na kuongeza ufanisi katika taaluma, malezi, ukarabati wa kituo na miradi ya uzalishaji mali.

Dira ni: Kuwa Taasisi ya KKKT ambayo ni chemchemu ya elimu na madili ya maisha mema ya Kikristo na inayoweza kujiedesha na kujitegemea.

Dhamira ni: Kuwaandaa wanajumuia ya LJS kitaaluma na kimaadili ili waweze kujinga na vyuo mbalimbali na kuwa watumishi na mawakili wema wa Kristo katika maisha yao.



2012 hadi sasa, Mchg. Abdiel Ndosi. Sekondari imehitimisha wanafunzi 2,309 wa kidato cha nne na kidato cha sita. Wanafunzi 916 wamehitimu Kozi ya Uongozi, Viongozi wa vijana 28, na viongozi wa wanawake 56.

Walimu wa shule ya Awali (Chekechea-Kimontessori) 370 wamehitimu hapa. Wageni wengi wamejifunza lugha ya Kiswahili na maelekezo. Usharika wa kituo unatoa huduma za kiroho na ibada.

Ili kuinua uchumi wa kituo tunayo miradi ya ng'ombe wa maziwa, nguruwe na kuku wa mayai.

Kwa maelezo zaidi mwandikie Mkurugenzi:

Barua pepe: director\_ljs@yahoo.com

# Halmashauri kilele cha jubili



*Halmashauri ya Vijana KKKT ambayo itazinduliwa rasmi wakati wa kilele cha miaka 50 ya KKKT. Wa kwanza kushoto ni Mratibu wa Vijana KKKT, Mch. Anza Amen Lema, akifuatiwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Bw. Ebenezer Shao na Katibu, Sista Kokubanza Kiiza. Wa pili kulia ni Katibu Mkuu wa Kanisa la Kiunjili la Kilutheri Tanzania, Bw. Brighton Killewa.*



*Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa na Bibi Happiness Geffi Mwandishi wa Kanisa wakionekana wakati wa mukutano wa Kamati ya Utendaji hivi karibuni.*



*Kazi ya Injili ni kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho. Baadhi ya washirika wakitoka ibadani mjini Shinyanga.*



**Upasuaji wa magoti na nyonga waanza ALMC**

*Wawakilishi wa hospitali ya 'Arusha Lutheran Medical Centre' (ALMC) wakiongozwa na Profesa Mark Jacobson (kushoto) wakieleza hivi karibuni kuhusu kuanza kwa huduma ya upasuaji magoti, nyonga pamoja na fistula katika hospitali hiyo kwa kushirikiana na CCBRT na Vodacom. Wagonjwa wanasiadiwa usafiri na huduma ya tiba. Washirika wa mpango huu wanahamasisha na kuwaelekeza wagonjwa mahali pa kupata huduma hizo.*



*(Kushoto) Kanisa la kwanza kujengwa Dayosisi ya Iringa eneo la Pommerin.*

## Mwanamke wa kwanza kubarikiwa kuwa Mchungaji KKKT

*Na Mch. Sadataley Kurwa*

Miongoni mwa mambo ya kukumbukwa katika Dayosisi Iringa ni lile la tarehe 20/11/1991 ambapo Dayosisi iliweka historia mpya baada katika Kanisa la Kiunjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ya kumbariki Mtheolojia Tuseline Kihwele Madembo kuwa mwanamke wa kwanza Mchungaji.

Historia hiyo ya kipekee imerudiwa tena mwaka 1998 ambapo. Mch. Agnes Kulanga amekuwa Mkuu wa Jimbo mwanamke wa kwanza katika Dayosisi ya Iringa. Mchungaji Agnes Kulanga ana historia ndefu katika Kanisa kwakuwa alishiriki Mkuutano Mkuu wa kwanza wa KKKT mwaka 1963 huko Bukoba uliojadili na kuunganisha makanisa saba na kuunda KKKT. Wakati huo aliwakilisha vijana wa Ukanda wa Kusini. Hadi kufikia mwaka 2012 Dayosisi ya Iringa ina wachungaji wanawake 34. Idadi ya wachungaji wanawake ni 200 kati ya wachungaji wote 2,000 wa KKKT.

# Ubatizo ni alama muhimu ya Ukristo

**Mchg. Kulwa Sadataley**

Neno ‘*ubatizo*’ linatokana na neno la Kigiriki: ‘*baptizo*’ ambalo maana yake ‘*naazimisha majini*’, ‘*naosha*’ lakini pia ‘*nanawa*’. Ubatizo ni Sakramenti ya kwanza ya Ukristo. Na unaitwa ‘*mlango wa sakramenti*’, kwa sababu ni lazima kubatizwa kabla ya kupokea Sakramenti ya “*Chakula cha Bwana*” yaani Mkate na Divai.

Ubatizo si maji matupu tu bali ni *maji yatumikayo kwa amri ya Mungu na yaliyounganika na Neno lake likiwa na lengo la kumzika mtu ili afufuke pamoja na Yesu Kristo katika uzima mpya*. Pia ubatizo una lengo la kumtakasa mtu kutoka dhambi zake. Ubatizo unaondoa makosa na unatuondoa katika kufa na katika nguvu ya Shetani. Pia unawapa uzima wa milele watu wote wanaoamini (*aaminie na kubatizwa ataokoka, asiy e amini atahukumiwa*). Na ni ushahidi wa nje wa yale yaliyotendeka ndani ya maisha ya mwenye kuamini. Ubatizo hufanyika kwa maji kama ishara ya usafi na ya uhai unaopatikana kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

“*Nami nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi; nitawatakaseni na uchafu wenu wote, na vinyago vyenu vyote. Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu,*” (Ez 36:26-27). “*Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenyewe kung’aa kama bilauri, ukitoka katika kitu cha enzi cha Mungu, na cha Mwanakondoo,*” (Ufu 22:1).

Nukuu toka *Tumwabudu Mungu Wetu* toleo 2012 inasema: “*Tujue na kutubu kila siku kusudi yule Adam wa kale akaaye ndani yetu ateswe, afe pamoja na dhambi zote na tamaa mbaya mle moyoni, naye aendelee mbele ya Mungu katika haki na utakaso pasipo mwisho.*”

Suala kwamba yawe maji mengi au machache si muhimu. Na hii inadhihirika tangu mwanzo wa Kanisa. Ubatizo ulitegemea mazingira na si vinginevyo. Kutokana na umuhimu wa Sakramenti hiyo Bwana Yesu ametuagiza *twende kubatiza watu duniani kote*. Mfano Paulo alipokuwa ndani ya nyumba “*akasimama akabatizwa*,” (Mdo 9:18). Na Yohane Mbatizaji katika Yoh 3:23 tunaona hakusogea mbali na mto Yordani, akisubiri watu wamuendee kutoka maeneo yote ya nchi ile kame awabatize.

Mwenye kubatizwa lazima awe

anamwamini Yesu Kristo kama mwokozi na kwamba lazima afahamu umuhimu wa ubatizo. Kama mtu ana mtambua Yesu Kristo kama mwokozi wake na ana ufahamu juu ya maana halisi ya ubatizo wa kikristo, kama njia ya heshima ya kudhihirisha waziwazi imani yake juu ya kristo, akitaka kubatizwa hakuna pingamizi yo yote. Kulingana na Biblia, ubatizo wa kikristo ni muhimu kwa sababu ni hatua ya heshima - kudhihirisha waziwazi imani yako juu ya Kristo na kuwajibika kwako kumfuata Yeye kwa

anaopaswa atimize ndipo abatizwe.

Injili ya Yohana inashuhudia Yesu pia alianza kubatiza, tena watu wengi kuliko Yohana, ingawa kwa njia ya wanafunzi wake (Yoh 3:22; 4:1-2). Baada ya kufufuka aliwaagiza *wakabatize mataifa yote: “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu,”* (Math 28:19).

Watoto wachanga wanaweza kubatizwa kwa sababu *hawakatai neema ya Mungu*. Wanafunzi wa Yesu walipotaka kuwazuia wasiletwe kwake “*akawaambia, Waacheni watoto wadogo waje kwangu, msiwazie; kwa maana watoto kama hawa ufalme wa Mungu ni wao. Amin, nawaambieni: Yeyote asiyekubali ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hatauinginga kabisa,*” (Mk 10:14-15).

Johannes Triebel anaandika katika kitabu: “*Kukiri Imani Mafafanuzi ya Mafundisho ya Ungamo la Augsburg*” kwamba ubatizo ni tendo la Mungu anayependa kuwatendea watoto pia, kwa njia hiyo tunawaweka katika milki ya Mungu wasibaki katika milki ya wazazi tu.

Ingawa watoto wachanga hawawezi kuelewa kinachofanyika, Mungu anaweza kuwamiminia rohoni mwanga wa imani. “*Vinywani mwa watoto wachanga na wanyonyao umeiweka misingi ya nguvu,*” (Zab 8:2). Hata watu wazima hawawezi kuelewa sakramenti kwa dhati, kwa kuwa zote ni mafumbo yanayotuzidi. Basi, kama Petro alipooshwa miguu, tumuachie Bwana atufanyie kazi anavyojuia Yeye. “*Nifanyalo wewe hujui sasa; lakini uthalishamu baadaye,*” (Yoh 13:7).

Kisha kuoshwa tuzidi kuchimba mafumbo hayo kwa mwanga wa Neno na wa Roho Mtakatifu. “*Je, mmelewa na hayo niliyowatendea?... Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo,*” (Yoh 13:12,15).

Kumbe, imani ya watu wazima inaweza kufaidisha watoto kama wengine pia. Walimletea Yesu “*mtu mwenye kupooza, anachukuliwa na watu wanne... Yesu, alipoiona imani yao, akamwambia yule mwenye kupooza, ‘Mwanangu, umesamehewa dhambi zako,*” (Mk 2:5). Kwa ubatizo watoto wanaunganishwa naye na kuanza kuponywa madonda ya dhambi ya asili.



**Mchg. Kulwa Sadataley**

kujitambulisha naye katika kufa kwake, kuzikwa na kufufuka. Na ubatizo lazima ufanywe na Mchungaji au mtu aliyepewa mamlaka kubatiza.

Yohana Mbatizaji aliwatikisa Wayahudi wenzake kwa kuhubiri toba kando kando ya Mto Yordani aliwadai wapokee “*ubatizo wa maji*” kama ishara ya kuongoka na ya kuwa tayari kumpokea Masiya ajaye, atakayebatiza “*kwa Roho Mtakatifu na moto,*” (Math 3:11).

Yesu aliagiza tubatize “*kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu*” (Math 28:19). Maneno hayo ndiyo muhimu zaidi katika sakramenti hiyo. Maji peke yake hayatoshi, hata yakiwa mengi, yanaweza kuosha mwili, lakini si roho. Kumbe ubatizo unaotuokoa “*siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu,*” (1Pet 3:21).

Yesu alibatizwa na Yohana akiwa na umri wa miaka 30 hivi akithibitisha ubora wa kazi ya mtangulizi wake na utayari wa kubeba dhambi za ulimwengu kama mwanakondoo wa sadaka ya upatanisho. Kwa maneno mengine hakuna katazo la ubatizo kwa kigezo cha umri. Maana hakuna umri maalum mtu

# Upendo FM 107.7



*Amani kwa wote*

JE UNAFAHAMU KITUO BORA CHA REDIO KATIKATI YA JIJI?

Kwa matangazo ya biashara na mikutano ya Injili,  
kwa ushauri wa kiroho na maendeleo ya jamii:  
Tangaza kwenye Redio bora ya Upendo na Amani  
kwa wote.

Fika sasa LUTHER HOUSE  
GHOROFYA PILI  
SOKOINE DRIVE.

Upendo FM 107.7 Mhz  
P.O. Box 13603  
Da es Salaam, Tanzania

Simu: 022 212 4228/ 2139556/ 2124221

E-mail: upendofm@yahoo.com

## Radio Furaha 96.7 FM

**Sikiliza matangazo ya  
kituo bora cha Redio Iringa  
na maeneo jirani.**

Kwa maoni, ushauri wa kiroho  
na kijamii wasiliana na:

**Meneja: Protas Kanemela**  
**Simu: +26 27 003 43**

**Fax: +255 262 701 198**

**Barua pepe: elctrdrd1987@yahoo.com**



## Ifahamu

### RADIO SAUTI YA INJILI

FM 92.2 & 96.2 MHz  
MOSHI

RSYI ni rafiki anayekujali kiroho na kimwili.

Katika Masafa ya FM, Radio Sauti ya  
Injili kutoka Moshi inasikika vizuri  
kabisa katika Masafa yafuatayo:

Moshi	92.2 MHz	Mlalo (Lushoto)	102.6 MHz
Arusha	96.2 MHz	Kisosora (Tanga)	96.7 MHz
Same	100.4 MHz	Morogoro	96.6 MHz
Kibaya (Kiteto)	102.9 MHz	Hakwe (Rombo)	96.4 MHz

Aidha Radio Sauti ya Injili, Moshi inasikika kwenye  
tovuti dunia nzima kwa saa 24

[www.sautiyainjili.org](http://www.sautiyainjili.org)

Radio Sauti ya Injili inatangaza vipindi  
mbalimbali vikiwemo vya maendeleo,  
afya, uchumi, habari na halikadhalika  
vipindi vya mafundisho ya dini. Unaweza  
kupata habari moto moto za kitaifa na  
kimataifa katika kipindi cha Dira ya Leo.

**Wasiliana na:**

**Mkurugenzi RSYI**  
**S.L.P. 777, Moshi**

**Simu: 027 27 52772 au 027 27 53080**

**E-mail: redio@elct.org**

**Tovuti: [www.sautiyainjili.org](http://www.sautiyainjili.org)**

Kumbuka kuwa RSYI ipo kwa ajili yako. Aidha,  
kijamii. Endelea kuimarisha huduma nzuri hii kwa  
hali na mali.

**The Board,  
Management and Staff  
of the New Safari Hotel  
(1967) Ltd**

wish to congratulate  
the Evangelical Lutheran  
Church in Tanzania (ELCT)

**on this auspicious  
occasion of the  
Jubilee celebrations  
(50 years since  
it came into being  
after uniting 7  
Lutheran Churches  
in Tanzania).**

The New Safari  
Hotel is privileged  
to commemorate with  
ELCT members this  
important milestone in  
the Church history.



**NEW SAFARI HOTEL (1967) LTD**

With over 46 Rooms, 4 Conference Halls, 3 Restaurants  
and an Internet Cafe...

...WE'VE GOT IT ALL!



P.O. Box 303, Boma Road, Arusha, Tanzania  
T: +255 254 5940/1 F: +255 272 548 318  
E: newsafarihotel@habari.co.tz